Nipashe MIAKA 30 — Mwanga wa Jamii
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 29, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com 0677 020 710
ISSN 0856 • No. 0581906
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 3

**Apoteza** maisha akiogelea bwawani ' sikukuu ya Krismasi



UKURASA WA 3

**Chuo** Kikuu Mzumbe kinara kwa ulipaji kodi

UKURASA WA 11

MAISHA YALIVYO

**Mwanamume** Simama kwenye nafasi kuiponya ndoa yako




**Saka kurudi uwanjani Machi**

UKURASA 22

# AJALI ZILIVYOTIKISA 2024

UKURASA 4



UKURASA 2

## Dk. Mwinyi atangaza neema kwa wanafunzi elimu ya juu



## Watu sita wafariki dunia wakienda kwenye usaili

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

WATU sita wakiwamo walimu wanne wa Shule ya Msingi Lumalu, kata ya Upolo, Nyasa mkoani Ruvuma, wamefariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka katika kijiji cha Upolo kwenda Kilosa Mbambabay, kuungua moto.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Peres Magiri, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana saa 2:00 asubuhi katika eneo la kona za Chunya inapopita barabara inayotoka Mbinga - Mbambabay.

Alisema watu hao walipata ajali wakiwa njiani kwenda kwenye usaili wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) ya uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura. Gari hilo aina ya Toyota Prado liliacha njia na kugonga gema la barabara kisha kupinduka na kuwaka moto.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kilichosababisha watu hao kushindwa kujiokoa na kuungua moto ni milango ya gari hilo kujifunga.

"Jitihada mbalimbali zilifanyika, kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ilikwenda kwenye eneo la tukio kuona namna ya kuondoa miili ya marehemu hao na kuisafirisha kwenda hospitali ya serikali ya wilaya ya Mbinga kwa ajili ya taratibu za kufanya uchunguzi wa vinasaba (DNA) ili miili ikabidhiwe kwa ndugu zao," alisema.

ENDELEA UKURASA 2

MICHEZO YANGA KUWAPA MASHABIKI ZAWADI YA KUFUNGA MWAKA UK.24 MAONI, UK.6

# Sita wafariki dunia gari likiwaka moto

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

WATU sita wakiwamo walimu wanne wa Shule ya Msingi Lumalu, kata ya Upolo, Nyasa mkoani Ruvuma, wamefariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka katika kijiji cha Upolo kwenda Kilosa Mbambabay, kuungua moto.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Peres Magiri, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana saa 2:00 asubuhi katika eneo la kona za Chunya inapopita barabara inayotoka Mbinga - Mbambabay.

Alisema watu hao walipata ajali wakiwa njiani kwenda kwenye usaili wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) ya uandikishaji wa daftari la kudumu la wapigakura. Gari hilo aina ya Toyota Prado lilіacha njia na kugonga gema la barabara kisha kupinduka na kuwaka moto.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kilichosababisha watu hao kushindwa kujiokoa na kuungua moto ni milango ya gari hilo kujifunga.

"Jitihada mbalimbali zilifanyika, kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ilikwenda kwenye eneo la tukio kuona namna ya kuondoa miili ya marehemu hao na kuisafirisha kwenda hospitali ya serikali ya wilaya ya Mbinga kwa ajili ya taratibu za kufanya uchunguzi wa vinasaba (DNA) ili miili ikabidhiwe kwa ndugu zao," alisema.

Magiri aliwataja waliofariki dunia kuwa ni dereva na mmiliki wa gari hilo, Vincent Milinga, na walimu Damas Nambombe, Dominika Ndau, Judith Nyoni, Sylvester Mtuhi na mfamasia Boniface Mapunda.

Jitihada za kumpata Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya, kuzungumzia suala hilo ziligonga mwamba baada ya kupigiwa simu zaidi ya mara mbili bila kupokewa.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mwendesha baiskeli akiwa amepakia madumu akienda kufanya biashara akipita barabara ya Morogoro Manzese jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwinyi atangaza neema mikopo elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk, Hussein Ali Mwinyi, ameiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha wanafunzi wote wenye sifa wanapatiwa mkopo ili kuendelea na elimu ya juu kwa wakati.

Dk. Mwinyi ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) alisema hayo jana alipowatunuku vyeti wahitimu wa ngazi mbalimbali katika mahafali ya 20 ya chuo hicho yaliyofanyika katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein, Tunguu, Wilaya ya Kati mkoa wa Kusini Unguja.

Dk, Mwinyi alisema kwa kutambua umuhimu wa elimu, serikali itaendelea kuchukua kila juhudi kuhakikisha mazingira bora ya upatikanaji wa elimu kwa ngazi zote ili kuwa na wana taaluma wenye weledi , ujuzi utakaochochea maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Rais Dk, Mwinyi alieleza kufarijika na ongezeko la wahitimu wa chuo hicho kila mwaka hatua inayoakisi dhamira ya chuo ya kuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi.

Alisema kumekuwa na ongezeko la asilimia 8.4 la wahitimu mwaka 2023/24 kwa wahitimu 2,291 kulinganisha na wahitimu 2,101 mwaka uliopita pamoja na ongezeko la wahitimu wanawake kwa asilimia 61 na kuwataka kuwa sehemu ya mabadiliko chanya kwenye maendeleo ya jamii .

Dk, Mwinyi alisema serikali imetenga Sh. bilioni 33.4 kwa ajili ya mikopo na wanafunzi 8.870 wanaotarajiwa kupatiwa mikopo hiyo.

Aidha, alisema serikali itaendelea kuandaa programu mbalimbali katika taasisi za kitaaluma za ndani ya nchi na kimataifa ili kuinua kiwango cha taaluma kwa wataalamu, wafanyakazi na wanataaluma wa SUZA ili kuongeza hadhi ya chuo na kuwa chenye kutoa elimu bora.

Alisisitiza kuwa lengo ni kuwa na chuo kinachotoa wahitimu wenye sifa, weledi na ujuzi watakaohimili ushindani katika soko la ajira au kujiajiri na kuendana na kasi ya maendeleo iliyopo hivi sasa

Dk. Mwinyi alibainisha kuwa serikali imejikita katika kuimarisha ubora wa elimu kwa kutoa mafunzo endelevu kwa wanataaluma na watumishi waendeshaji wa SUZA kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa ili kuleta programu bora na zinazokidhi viwango vya kimataifa.

Alilipongeza Baraza la Chuo hicho kwa kufundisha shahada ya sayansi ya utabibu ya kinywa na meno na kuanzisha programu zingine mpya nne za elimu chuoni hapo zikiwamo Shahada ya Elimu Jumuishi na Mahitaji Maalum ya Kielimu, Shahada ya Elimu ya Amali na Shahada ya Elimu na Lugha pamoja Shahada ya Mafunzo ya Ubaharia inayotarajiwa kuanza kufundishwa mwaka 2025.

Rais Dk, Mwinyi alisema hatua hiyo itaiwezesha serikali kuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta mbalimbali watakaotoa mchango wao katika Maendeleo ya kijamii.

Aidha, Rais Dk, Mwinyi alimtunuku Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais ,Katiba, Sheria ,Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa ya Elimu ya Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA).

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Moh'd Mussa, alisema chuo hicho kimekuwa alama maalum ya utambulisho wa Zanzibar kitaaluma kwa mafanikio ya kutoa wahitimu na taaluma bora.

Alieleza fursa ya kuwapo kwa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya diploma kumeongeza idadi ya wanafunzi kujiunga na chuo hicho kwa ngazi hiyo na kuahidi wizara hiyo kuhakikisha chuo kinaimarika na kupata hadhi kimataifa.

Makamu Mkuu wa SUZA, Prof. Makame Haji, alisema mipango bora ya serikali na miongozo, busara na hekima za Rais Dk. Mwinyi zimekuwa kichocheo cha mabadiliko na maendeleo makubwa ya chuo hicho.

Alisema kutokana na ongezeko la wahitimu, chuo kina mpango kuendesha miradi tofauti ya upanuzi wa miundombinu ya majengo kwa kuwa na majengo ya ghorofa kupitia mpango wa mkuu wa chuo hicho.

Hatua hiyo itaambatana na ujenzi wa maabara ya sayansi ,Skuli ya Kilimo, Skuli ya Elimu ya Lugha za Kigeni, ujenzi wa Skuli ya Afya, Sayansi na Tiba ikiwa miongoni mwa miradi

Zaidi ya wahitimu 2,200 wa ngazi ya vyeti, stashahada, shahada, na shahada ya uzamili na uzamivu walitunukiwa vyeti vyao katika mahafali hayo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## HABARI KITAIFA

# Aokotwa mtaani amefariki dunia

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

MWANAMKE mmoja anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 25 hadi 30 amekutwa akiwa amefariki dunia katika eneo la Mtaa wa Mtakuja Kata ya Mwisenge Manispaa ya Musoma mkoani Mara.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Pius Lutumo, alisema mwili wa marehemu huyo uliokotwa ukiwa hauna jeraha Desemba 28, majira ya saa 10:00 asubuhi katika eneo lenye uwazi mtaani hapo.

"Hadi sasa waliofika eneo la tukio hawakuweza kumtambua marehemu huyo na mwili wake umehifadhiwa katika Hospitali ya Manispaa ya Musoma," alisema.

Kamanda Lutumo alisema Jeshi la Polisi linafanya uchunguzi juu ya kifo cha mwanamke huyo ili kubaini utambulisho wake sambamba na chanzo cha kifo chake.

Kamanda Lutumo alitoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Mara kuendelea kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu kabla ya matukio hayajatokea, ili wahusika waweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria za hapa nchini.

# Apoteza maisha akiogelea wakati wa Krismasi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

MKAZI wa Mtaa wa Bukondamoyo, Kata ya Mhungula, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Mbaraka Magese (24), amekutwa amefariki dunia akiwa kwenye bwawa la kuogelea siku ya Sikukuu ya Krismasi.

Mwili wa marehemu ulikutwa ukielea katika bwawa hilo lililoko katika baa ya Nzengo Grill, Mtaa wa Mbulu, kata ya Mhongolo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho na kuwa mpaka sasa wanamshikilia msimamizi wa bwawa hilo kwa uchunguzi zaidi.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini Magese alifariki dunia akiwa anaogelea huku mvua inanyesha na alizidiwa baada ya kunywa maji mengi.

Aidha, Magomi aliwataka wamiliki wa kumbi za starehe pamoja na maeneo ya kuogelea kuwa waangalifu pia kufunga mabwawa ya kuogelea wakati mvua ikinyesha ili kuepusha madhara kama hayo.

Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kahama, Stanley Luhwago, alisema wasimamizi wa mabwawa hayo lazima wawe na ujuzi wa kuogelea pamoja na vifaa vya kuogelea kama majaketi na maboya ili kuhakikisha usalama kwa waogeleaji kwa kuwa wako wengine hawajui kuogelea kabisa na michezo hiyo wanaitamani.

Alisema ili kuondoa majanga hayo kuendelea kutokea, wamejipanga kuwatembelea wamiliki wa mabwawa hayo pamoja na wasimamizi wao kuwapatia elimu ya kuwakinga na majanga wateja wao na kuhakikisha hakuna uogeleaji unaweza kufanyika wakati wa mvua.

"Ni ngumu kumtambua mtu asiyejua kuogelea kwenye mabwawa haya lakini ni rahisi kudhibiti majanga haya yasitokee kwa sababu msimamizi alipaswa kumzuia marehemu kuogelea kutokana na mvua iliyokuwa inanyesha siku hiyo.

"Tuendelee kuzingatia matakwa ya kisheria tunayowapatia kabla ya kujenga mabwawa haya," alisema Luhwago.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, ameagiza baa hiyo ifungwe kutokana na kutokidhi vigezo vya usalama katika huduma za kuogelea na upelelezi ukikamilika na kubainika kuna uzembe ulitendeka, mmiliki wake achukuliwe hatua za kisheria.

Alisema wamiliki wa mabwawa ya kuogelea wanapaswa kuzingatia sheria na kanuni zinazohusiana na uendeshaji wa mabwawa ili kuepuka majanga kama hayo na wale watakaobainika wachukuliwe hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufungiwa mabwawa hayo kuendelea kufanya kazi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Mhitimu wa Chuo cha Abundant Wold Bible College Ohio U.S.A, Irene Mashine, akibusu shada la maua alilokabidhiwa na familia yake baada ya kutunukiwa shahada ya Udaktari wa heshima ya Uongozi katika mahafali ya 8 ya Chuo hicho yaliyofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Chuo Kikuu Mzumbe kinara ulipaji kodi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imekitaja Chuo Kikuu Mzumbe (MU) kilichoko mkoani Morogoro kuwa kinara katika ulipaji wa kodi kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2024.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Utafiti na Sera wa TRA, Dk. Ephraim Mdee, mjini hapa wakati wa kukabidhi cheti cha pongezi na kutambua mchango wa chuo kikuu hicho katika ulipaji wa kodi.

Dk. Mdee alisema mamlaka hiyo inatambua na kuthamini taasisi zinazolipa kodi ya serikali kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

"Nachukua nafasi hii kukipongeza sana Chuo Kikuu Mzumbe. Mmekuwa kinara katika ulipaji wa kodi. Tunashirikiana nanyi na mmekuwa mstari wa mbele katika hili," alisema.

Dk. Mdee alisema Desemba kila mwaka,

TRA imekuwa ikifanya matendo ya kutoa shukrani kwa walipakodi wazuri nchini kwa kutambua mchango wao na kuwapatia vyeti nchini kote .

Alisema mkoa wa Morogoro umefanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato na unaendelea kufanya vizuri.

Dk. Mdee alisema miezi mitano iliyopita kufikia Novemba 2024, mamlaka hiyo mkoani Morogoro ilifikia lengo la asilimia 102 na kutokana na ushirikiano unaooneshwa na walipakodi.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Prof. Allen Mushi, alisema Mzumbe imejikita katika kufundisha masuala ya uongozi, fedha, sheria na biashara, hivyo ni lazima yanayofundishwa darasani yaendane na vitendo .

"Yale tunayofundisha darasani yanaendana na vitendo. Tunawafundisha wanafunzi wetu masuala ya uongozi, uwajibikaji, nidhamu, haki na wajibu," alisisitiza Prof. Mushi.

Mbali na chuo hicho, viongozi wa mamlaka hiyo walitembelea wafanyabishara kadhaa wakiwamo wa Soko la Chifu Kingalu, Manispaa ya Morogoro.

Baadhi ya wafanyabiashara, akiwemo Mwenyekiti wa Machinga Mkoa wa Morogoro, Faustine Francis, waliishauri mamlaka hiyo kupanua wigo wa utoaji wa elimu ya kodi kwa wananchi na wafanyabiashara walioko maeneo yanayokua kibiashara.

Mwenyekiti huyo alisema lengo ni kuwawezesha wawe na uelewa zaidi na ili hatimaye waone umuhimu kwao kulipa kodi kwa hiari kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Watanzania wote .

Mamlaka hiyo imesogeza huduma kwa wafanyabiashara na kuweka vituo vya utoaji wa namba ya mlipakodi (TIN) na namba ya malipo ya kodi kwenye Soko Kuu la Chifu Kingalu na ofisi ya Kata ya Kihonda, Manispaa ya Morogoro.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

UCHAMBUZI

# Ajali zilivyotikisa 2024

## -Mamia wapoteza maisha, uzembe wa madereva chanzo kikuu




**Na Waandishi Wetu**

AJALI, ajali, ajali. Huo ulikuwa sawa na wimbo uliochukua chati ya juu kwa mwaka 2024 kutokana na matukio ya ajali yaliyotokea katika maeneo mbalimbali nchini.

Januari hadi Desemba kumekuwa na matukio hayo ambayo yamesababisha mamia ya watu kupoteza maisha, wengine kujeruhiwa na baadhi yao kupata ulemavu wa kudumu sambamba na upotevu wa mali na uharibifu wa vyombo vya moto. Kwa jumla, hakuna mkoa ambao haujaguswa na matukio ya ajali katika mwaka 2024.

Wakati zikiwa zimebaki siku chache kutamatika kwa mwaka 2024, matukio kama hayo yametokea wakati Watanzania wakiwa katika shamrashamra za Krismasi.

Desemba 24, mwaka huu, watu 11 walifariki dunia papo hapo na wengine 13 kujeruhiwa katika wilaya ya Handeni mkoani Tanga, ajali iliyohusisha gari la mizigo Mitsubishi Fuso lililokuwa likitoka Lushoto kwenda Dar es Salaam na Toyota Coster ikitoka Handeni kwenda Tanga mjini.

Ajali hiyo ikiwa haijatoka katika akili za Watanzania, Desemba 26 ikatokea ajali nyingine Tarakea, Rombo mkoani Kilimanjaro iliyohusisha basi la kampuni ya Ngasere na Toyota Noah. Katika ajali hiyo, watu 10 walipoteza maisha na wengine kujeruhiwa.

Tangu kuanza kwa mwaka huu, ajali zimekuwa jambo la kawaida licha ya serikali kupitia Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, kuwaonya madereva kwa kushindwa kufuata na kuheshimu sheria za usalama barabarani. Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wakuu wa kitaifa wamekuwa mara kwa mara wakitoa maagizo kuhusu udhibiti wa ajali lakini maagizo hayo yamekuwa kama sikio la kufa.

### VIFO 102 KANDA YA ZIWA

Katika kanda ya Ziwa, ajali zilizoripotiwa kuanzia Januari mpaka jana, zilisababisha vifo 102 huku ajali za barabarani zikiongoza kwa kusababisha vifo 82.

Jinamizi la ajali katika ukanda huo, lilianzia Januari 13, baada ya watu 22 kufukiwa na kifusi na kufariki dunia. Hatua hiyo ilisababisha Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, kutangaza kufunga machimbo hayo na kuwataka wachimbaji kuunda vikundi ili visajiliwe wizarani.

Januari 30, katika Manispaa ya Shinyanga, Daudi Mwandu (25) mkazi wa Bugweto aligongwa na gari aina ya Toyota Land Cruiser lenye namba za usajili T. 952 BSP na kufariki dunia huku abiria wake, Mtatiro Wambura (33), akijeruhiwa.

Baada ya ajali hiyo wananchi waliandamana kutaka udhibiti wa kasi za madereva na kulishinikiza Jeshi la Polisi kumkamata dereva wa gari hilo aliyekimbia na gari. Kamanda wa Polisi mkoani humo, Janeth Magomi, alifika katika eneo la tukio kutuliza hasira za wananchi na kuwasihi kwamba serikali imesikia kilio chao.

Mkoani Kagera, ajali ya basi la shule binafsi ya Kemebos ilisababisha kifo cha mwanafunzi kidato cha tano, Frank Makage, na wengine kujeruhiwa lilipokuwa likisafirisha wanafunzi kwenda likizo.

Aprili 24, mkoani Mwanza katika eneo la Daraja la Mwananchi, majira ya saa 1;20 asubuhi, gari lenye namba za usajili T 744 DCG Toyota Hiace lililokuwa limebeba wanafunzi wa Shule ya Msingi Mchepuo wa Kiingereza Nyanza, lilifeli breki na kusababisha kifo cha mtu mmoja huku wengine watano wakijeruhiwa.

Ajali nyingine ilitokea Juni 27, majira ya saa 12:15 jioni wilayani Chato, mkoani Geita ambayo ilisababisha watumishi wawili wa afya kupoteza maisha baada ya kugongwa na gari aina ya Toyota Probox wakiwa kwenye pikipiki wakitoka kwenye njia ndogo kuingia kwenye barabara kubwa pasipo kuchukua tahadhari.

Ajali nyingine iliyotokea huko mkoani Simiyu ilisababisha vifo vya watu watatu wa familia moja na ng'ombe sita ikihusisha basi la kampuni ya Ally's na Mitsubishi Fuso.

Taarifa ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Edith Swebe, ilitaja chanzo cha ajali hiyo iliyotokea katika Kijiji cha Ruguru wilayani Itilima kuwa ni mwendokasi na dereva wa Fuso aliyejaribu kupishana na magari bila kuchukua tahadhari.

Wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, lori lenye namba za usajili T.854 DBY na tela namba T.180 DVH liligongana na gari lenye namba T.195 EEY na tela namba T.811 SYU lililokuwa likitokea Bukoba na mzigo wa kahawa na kuwaka moto na kusababisha vifo vya watu watatu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga Janeth Magomi alisema chanzo cha ajali hiyo ni lori lililokuwa likiendeshwa na Rajab Tabu likilikwepa gari la mchanga bila kuchukua tahadhari.

Basi la Kampuni ya Nyehunge likitokea Morogoro kwenda Mwanza, liliacha njia na kugongana na basi la Asante Rabi lililokuwa likitokea Mwanza kwenda Arusha katika eneo la Ukiruguru wilayani Misungwi na kusababisha vifo vya watu wanane huku 39 wakijeruhiwa.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilbroad Mutafungwa, alisema chanzo chake ni mwendo kasi na dereva kuchepuka bila kuchukua tahadhari.

Wilayani Tarime, mkoani Mara Daniel Elias, na mke wake, Kadogo Daniel, walifariki dunia kwa nyakati tofauti baada ya kugongwa na lori lililokuwa katika mwendokasi wakiwa katika pikipiki kisha lori hilo kutokomea nchini Kenya.

Aidha, wilayani Bunda mkoani Mara, watu wanne walifariki dunia baada ya lori aina ya Mitsubishi Fuso lililokuwa limebeba mawe, kuacha njia na kuparamia wananchi na wafanyabiashara katika eneo la mataa kuacha njia na kugonga gereji

Katika wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, lori la mizigo aina ya Scania, liligongana na Toyota Hiace pamoja na Toyota Coaster katika eneo la Kihanga na kusababisha vifo vya watu saba na wengine tisa kujeruhiwa.

Kamanda wa Polisi mkoani humo Blasius Chatanda, alisema chanzo ni uzembe wa dereva wa lori kutochukua tahadhari na kuendesha gari kwa mwendo kasi.

Desemba 21, Kagera katika wilaya ya Biharamulo, basi la abiria Kampuni ya Capco One lilifeli breki katika mteremko na kusababisha vifo vya watu 11 huku wengine 42 wakijeruhiwa.

### TABORA NAKO

Juni 19 mkoani Tabora, basi la kampuni ya Mumuki liligongana na gari ndogo aina ya Toyota Hiace. Katika ajali hiyo, watu wawili, akiwamo Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Igunga, Zawadi Wiliam (60) walifariki dunia na wengine 12 walijeruhiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Richard Abwao, alisema ajali hiyo iliyotokea saa 7:00 mchana, ilisababishwa na dereva Richard Gabriel (42) aliyekuwa akijaribu kuyapita magari mengine matatu bila kuchukua tahadhari.

Ajali nyingine mkoani humo ilihusisha gari la abiria aina

INAENDELEA UK. 5

# Wajipanga kufunga mwaka kwa kuunga mkono juhudi za Samia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BONANZA la michezo Dk.Samia/ Jumbe Holiday,litafanyika katika Uwanja wa CCM Kambarage mjini Shinyanga Desemba 31, ambayo ni siku pia ya kufunga mwaka 2024 na kuukaribisha mwaka 2025.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa Mashindano ya Bonanza hilo, Jackline Isaro, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema katika bonanza hilo la michezo hakutakuwa na kiingilio chochote bali ni bure na hivyo kutoa wito kwa wananchi wa Shinyanga kwamba wajitokeze kwa wingi ili kuufunga mwaka 2024 kwa furaha na kuukaribisha mwaka 2025.

"Rais Dk. Samia Suluhu Hassan anahimiza michezo, hivyo kupitia mashindano haya tutaona vipaji mbalimbali, na itakuwa furaha kwa wakazi wa Shinyanga kufunga mwaka, na kuukaribisha mwaka mpya 2025," alisema Isaro.

Alitaja michezo ambayo itachezwa kwenye bonanza hilo kuwa ni mbio za baiskeli, mchezo wa bao, drafti, karata, ususi, Ps Game, netiboli, kikapu, kufukuza kuku kwa jinsia zote, kushindana kula, pool table na muziki.

Mashindano mengine, kwa mujibu wa mratibu huyo ni mpira wa miguu ambao utakuwa kati ya bodaboda na bajaji, bingwa wilaya 'Ranges' dhidi ya Ngokolo, na dabi ya upongoji.

Alizitaja zawadi za washindi kwamba katika mbio za baiskeli mshindi ambayo yatakuwa makundi manne zawadi ni Sh. milioni 2.1, bao mshindi wa kwanza Sh. 100,000, drafti Sh.100,000, karata Sh.100,000, msusi Sh.100,000, PS game Sh. Sh.200,000, wa pili Sh. 100,000 na watatu Sh. 50,000.

Mpira wa pete, washindi wa kwanza watapewa Sh.500,000, kreti saba za soda, mchele kilo 50, washindi wa pili Sh. 300,000, mchele kilo 50 na soda kreti saba.

Mpira wa kikapu kwa jinsia zote, mshindi wa kwanza atapa Sh.500,000 na wa pili Sh.300,000.

Kwa mchezo wa kufukuza kuku kwa jinsia zote, washindi wa kwanza watapa kuku na Sh. 20,000 na mchezo wa kula washindi wa kwanza watapata Sh. 20,000, huku mchezo wa pool table mshindi wa kwanza ataibuka na kitita cha Sh. 100,000na wa pili Sh. 50,000.

Kwa upande wa mpira wa miguu timu ya bodaboda dhidi ya bajaji, mshindi wa kwanza atapata Sh. 500,000, Ng'ombe mmoja, kreti saba za soda na mchele kilo 100, wa pili Sh.300,000, ng'ombe mmoja na mchele kilo 100.



Mkuu wa Shule ya Baybridge, Bijal Chandarana, akimkadhi cheti Mwanafunzi wa Shule hiyo, Jennifer Nerissa, wakati wa hafla ya kuchangisha pesa kusaidia watoto wenye saratani iliyofanyika shuleni hapo jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajali zilivyotikisa 2024

**INATOKA UK. 4**

ya Toyota Hiace lililogongana na Mitsubishi Fuso. Katika ajali hiyo, watu 14 wakiwamo vichanga wawili walifariki dunia na wengine tisa walijeruhiwa.

Kamanda Abwao alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva kutaka kuchepuka na kujaribu kuyapita magari mengine akiwa kwenye mwendokasi.

**AJALI MBEYA**

Juni 5, ilitokea ajali mbaya katika Mteremko wa Mbembela jijini Mbeya baada ya lori aina ya Scania lililokuwa limebeba shehena ya kokoto likitokea Uyole kwenda Tunduma kufeli breki na kuyaparamia magari mawili, pikipiki na guta, hivyo kusababisha vifo vya watu 13 papo hapo na kujeruhi 18.

Lori hilo lilianza kuigonga gari ndogo aina ya Harrier yenye namba za usajili T. 120 DEL na kupoteza mwelekeo kwenda kuligonga gari aina ya Toyota Coaster lililokuwa likitoka Tunduma kwenda jijini Mbeya.

Ajali ya pili ilitokea katika Kijiji cha Itamboleo Kata ya Chimala wilayani Mbarali. Basi la Kampuni ya Shari Line lenye namba za usajili T. 896 DHK lililokuwa likitokea mkoani Rukwa kwenda Njombe, liliacha njia na kugonga gema kisha kuanguka.

Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu tisa na kujeruhi 18. Chanzo cha ajali kilielezwa kuwa ni uzembe wa dereva aliyekuwa akiendesha basi hilo. Alikamatwa na polisi baada ya ajali hiyo na kuchukuliwa hatua.

Septemba 6, ajali nyingine ilitokea katika Kijiji cha Lwanjilo, wilayani Mbeya ikihusisha basi la Kampuni ya AN CLASSIC lililokuwa likitokea Mbeya kwenda Tabora baada ya kuacha njia na kugonga gema kishakusababisha vifo vya watu 12 na kujeruhi wengine 36.

Ilibainika kuwa gari hilo lilikuwa limezimwa kidhibiti mwendo kwa zaidi ya mwezi hali iliyokuwa inasababisha madereva kuendesha kwa mwendokasi bila kudhibitiwa.

Ajali nyingine iliyogharimu maisha ya watu ilitokea Septemba 27, ambapo gari aina ya fuso lililokuwa limebeba abiria likitokea katika Mji wa Mbalizi kwenda kwenye Mnada wa Ilembo lilifeli breki na kupinduka katika Kijiji cha Jojo. Watu 12 walifariki dunia na 23 walijeruhiwa.

**DODOMA PIA**

Ajali ya gari iliyogonga treni ilisababisha vifo vya mume na mke katika makutano ya reli na barabara eneo la Medeli, jijini Dodoma huku binti yao wa miaka miwili aliyekuwapo kwenye gari hilo akinusurika.

Wanandoa hao, Mhandisi Hussein Chilala na Furaha Hamisi walipata ajali baada ya kugonga treni iliyokuwa inakwenda mikoa ya Tabora na Kigoma. Ajali hiyo ilitokea majira ya saa 2:00 usiku wa Aprili 4, 2024 wakati wanandoa hao wakienda kununua keki kwa ajili ya kumbukizi ya siku ya kuzaliwa ya binti yao.

Ajali nyingine ilitokea Desemba 7, 2024 katika eneo la Chinangali One, Barabara Kuu ya Dodoma-Morogoro, baada ya malori matatu kugongana na kusababisha msongamano mkubwa wa magari pamoja na madhara kwa vyombo vya usafiri vilivyohusika.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio, ajali hiyo ilihusisha malori matatu yaliyokuwa yakisafiri kwa kasi, moja liligongana na magari mengine yaliyokuwa yakiendelea na safari zao.

Aidha, zaidi ya wabunge 50 waliokuwa wakisafiri kwa basi kutoka Dodoma kwenda Kenya kushiriki michezo walipata ajali eneo la Mbande mkoani Dodoma. Wabunge kadhaa walipata majeraha ya mwili kutokana na ajali hiyo.

Basi hilo la Bunge likiwa katika mwendo wa kawaida lilikutana na changamoto ya gari lingine lililokuwa limeangusha mizigo barabarani na wakati dereva akijaribu kukwepa mizigo hiyo, ndipo basi hilo lilipoacha njia na kuingia porini.

Miongoni mwa wabunge waliojeruhiwa ni pamoja na Jackson Kiswaga (Kalenga) Jesca Msambatavangu (Iringa Mjini) na wa Viti Maalum, Grace Tendega

**AJALI ZINGINE**

Katika mwaka huu pia, kulitokea ajali zingine ikiwamo ya boti ya mizigo Septemba 25, katika Ziwa Victoria eneo la Kirumba na kusababisha vifo vya watu tisa.

Ajali nyingine ilitokea Itilima mkoani Simiyu ikihusisha mabinti wanne waliofariki dunia baada ya kuzama kwenye dimbwi lililochimbwa kwenye makazi ya watu kwa ajili ya uchimbaji madini walipokwenda kufua na kuchota maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Watoto hao ni wa familia tatu tofauti ikiwa kati yao wawili ni wa familia mmoja na watatu ni wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lagangabilili walifariki dunia baada ya mwenzao kuteleza na kuzama katika dimbwi hilo na wao kuanza kujaribu kumwokoa.

Mkoani Tabora, mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi minane, Martin Ndalu, alifariki dunia na mwingine kujeruhiwa baada ya kupigwa na shoti kupitia waya uliokuwa ukishikilia nguzo ya umeme katika kata ya Kitete, Manispaa ya Tabora.

Katika mkoa wa Mwanza, watu wawili walifariki dunia kwa kupigwa na mshituko wa umeme 'shot' wakati wakihamisha nguzo kutoka kwenye Mradi wa ujenzi wa barabara jijini Mwanza.

Kamanda Mutafungwa alisema tukio lilitokea Agosti 10, 2024 majira ya saa 7:30 mchana katika Mtaa wa Semba wilayani Nyamagana.

Mkoani Kagera, watoto wawili wa familia moja, Justa John (9) aliyekuwa mwanafunzi wa darasa la kwanza Shule ya Msingi Mubembe na Juliethа John (4) wa Kitongoji Mubembe, Kijiji cha Lwagati wilaya ya Bukoba, walifariki dunia katika ajili ya moto baada ya nyumba walimokuwa wakiishi kuwaka na kuteketea.

Wilayani Nzega, mkoani Kagera watu watatu wamefariki dunia kwa kuangukiwa na ukuta wa nyumba na kusababisha vifo katika kijiji cha Iyombo Nyasa kata ya Utwigu.

Kamanda Abwao aliwataja marehemu hao kuwa ni Rashidi Matoma, Chiku Mihayo na Hamisi Rashid. Alisema watu hao walifariki dunia baada ya kuangukiwa na ukuta ambao ulijengwa kwa matofali ya tope katika chumba walichokuwa wamelala wakati wa usiku.

**-Imeandaliwa na Vitus Audax (MWANZA), Nebart Msokwa (MBEYA) na Pul Mabeja (DODOMA).**

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii itathmini malengo ya 2024, kupanga mwaka ujao

**ZIKIWA** zimebaki siku tatu kabla ya kuaga mwaka 2024 na kukaribisha mwaka mpya wa 2025, kuna mambo mengi yamefanyika kuanzia ngazi ya familia, jamii na taifa. Kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Kwa ujumla, kila unapoanza mwaka mpya, familia, jamii na taifa kwa maana ya serikali, taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali na ya dini, huweka malengo kwa ajili ya maendeleo kwa mwaka husika. Mipango hiyo huwa ama katika masuala ya uchumi au jamii kutegmeana na malengo inayojiwekea familia au taasisi husika.

Pamoja na kuwapo kwa mipango na malengo hayo, ni watu wachache ambao hutekeleza kikamilifu kwa zaidi ya asilimia 90 huku wengine wakiishia kupanga tu na kuweka kwenye mashubaka bila utekelezaji wowote. Katika kundi hilo la wasiotekeleza, wengi huishi au kufanya kazi kwa mazoea ili mradi mwaka umefika na kumshukuru Mungu. Huko ni kwenda kinyume na kusudi la Mungu kumleta mwanadamu duniani ili atimize wajibu kwa mujibu wa kipawa na uwezo wake aliopewa.

Aidha, wengine hutekeleza kwa vitendo mipango na malengo yao kwa asilimia fulani na kuna kundi kubwa la watu ambao hawafikii hata asilimia 50 ya yale waliyojiwekea kufanya kwa mwaka husika. Kundi la watu hao hubaki kunung'unika na kutoa visingizio vya kushindwa kwao huku wakiitwisha serikali au jamii ya wenye uwezo, wanaotekeleza malengo yao na kupata mafanikio.

Visingizio hivyo kwa sehemu kubwa huwa ni ukosefu wa fedha au fursa na wengine wamekuwa wakidai hawana watu wa kuwashika mikono. Pia watu hao wamekuwa wakikosa nidhamu ya matumizi ya muda na rasilimali walizo nazo ikiwamo kufanya mambo ya ovyo na anasa. Matokeo yake ni kuendelea kuishi katika lindi la umaskini ilhali kuna fursa kedekede zinazowazunguka.

Mwaka 2024 unamalizika, hivyo ni wakati wa watu kufanya tathmini ya malengo na mipango waliyojiwekea kwa kuangalia mafanikio na changamoto walizokumbana nazo pamoja na sababu zilizowafanya kutokufikia mahali walipokusudia. Sambamba na kufanya tathmini hiyo, pia ni wakati wa kuweka mipango na malengo ya mwaka mpya kwa ajili ya mambo ya kufanya ili kufikia ndoto za mafanikio.

Kuna msemo kwamba pasipo maono hapana kujizuia. Kwa maana ya msemo huo, hakuna mtu, jamii wala taasisi inayoweza kufikia upeo wa mafanikio bila kuwa na maono ambayo ndiyo mwanga wa kule ambako mtu au taasisi inataka kufika.


Ni dhahiri kwamba inawezekana watu wengi hawafikii malengo yao kutokana na kukosa vitendea kazi na rasimali kama vile fedha. Pamoja na ukweli huo, ni vyema watu wakabadili fikra na mawazo kwa mwaka 2025 badala ya kuendelea kuwa na sababu na visingizio na hatimaye kuzidi kutopea katika lindi la umaskini.

Kwa kuwa watu wanatarajia kuingia mwaka 2025, kwa mapenzi ya Mungu, ni vyema kuanzia mtu mmoja mmoja, familia na jamii kujiwekea malengo na kuyatekeleza kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa hatimaye kupata matokeo yenye viwango vya hali ya juu.

Kazi pekee, kama ambavyo imekuwa ikielezwa katika mawanda tofauti, ndiyo itakayomfanya mtu kupata mafanikio katika eneo lolote na kazi hiyo ni lazima iwe na mipango ikiambatana na utekelezaji. Wahenga wanasema kazi bila mpango ni vurugu na mipango bila utekelezaji ni vurugu zaidi, hivyo jamii inapopanga mipango kwa mwaka ujao, haina budi kutekeleza kwa ufanisi.

Ni vyema jamii ikaacha kuishi na kufanya mambo kwa mazoea badala yake ichukue hatua kwa kupanga mipango na kutekeleza kwa manufaa yao na taifa kwa jumla. Kwa kufanya hivyo, ni dhahiri mafanikio yatapatikana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Karibu 2025 uwe wa kukomesha utoro kidato cha kwanza

Na Sabato Kasika

**MWAKA** 2024 unaelekea ukingoni ukiandaa kuupisha mwaka mpya wa 2025 ambao utaanza safari ya siku 365 Jumatano ijayo.

Wakati mwaka mpya ukiwa mbioni kuanza, ni vyema kuwakumbusha mambo kadhaa wanafunzi, wazazi na walezi ili yale ambayo huwa yanajitokeza kila mwanzo wa mwaka yasijirudie.

Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya wanafunzi wanaochagulia kuingia kidato cha kwanza kuwa watoro na kusababisha serikali kufanya msako ili kuwapeleka shuleni.

Mtindo huo unachangia kukwamisha maendeleo ya elimu kwa mwanafunzi kama utaendelea kujitokeza kila mwaka wa masomo bila wadau wa elimu kushirikiana na serikali kuukomesha.

Huwa inadaiwa kuwa wako baadhi ya wanafunzi huolewa baada ya kuhitimu elimu ya Msingi, wengine kubaki nyumbani wakiwasaidia wazazi wao shughuli mbalimbali.

Vilevile, wengine huhamishwa na wazazi wao kupelekwa shule zingine tofauti na zile walizopangiwa.

Hao sina tatizo nao bali wale ambao hukataa shule na kubaki wakichunga ng'ombe au kufanya shughuli yoyote ya nyumbani badala ya kusoma.

Ni wazi kwa hili wazazi au walezi ambao kimsingi ni wadau wa elimu, wanahusika moja kwa moja kukwamisha ndoto za watoto wao katika elimu, hivyo, tunapojiandaa kuanza mwaka mpya, ni vyema tatizo hilo liishie mwaka 2024 na kuanza ukurasa mpya usio na makandokando ya utoro.

> **Kwa ujumla ni kwamba utoro wa wanafunzi wa kidato cha kwanza hutokea kila mwaka nchi nzima na kuwalazimu viongozi wa serikali kuwakamata wazazi ambao watoto wao hawajaripoti shule.**

Kwa ujumla ni kwamba utoro wa wanafunzi wa kidato cha kwanza hutokea kila mwaka nchi nzima na kuwalazimu viongozi wa serikali kuwakamata wazazi ambao watoto wao hawajaripoti shule.

Iko mifano mingi lakini mfano wake ni huu wa wilayani Bukoba mkoani Kagera. Mwanzoni mwa mwaka huu unaoisha, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, Erasto Sima, alitangaza kuanzisha msako wa nyumba kwa nyumba ili kuwawajibisha wazazi na walezi ambao walishindwa kuwapeleka wanafunzi shuleni.

Alichukua uamuzi kwa kutoridhishwa na idadi ya wanafunzi waliofika shuleni kuanza kidato cha kwanza alipotembelea Shule ya Sekondari Samia Suluhu iliyopo Kata ya Kashai na kutaka wafike haraka.

Kwa mujibu wa Sima, wanafunzi ambao walichaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hiyo, walikuwa 98 wakiwamo wasichana 43 na wavulana 55.

Lakini hadi Januari 11, mwaka huu, wanafunzi waliofika shuleni walikuwa wavulana 14 tu na wasichana 10 huku idadi kubwa ya wazazi wakiwa hawajafika shuleni kutoa taarifa za watoto wao kuchelewa kuanza masomo.

Kwa kuwa tatizo ni la nchi nzima, ninadhani kuna haja kwa kila mkoa kujipanga kukabili tatizo hilo ili uwe mwisho wa kuwapo wanafunzi watoro wa kidato cha kwanza kila mwaka.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Kwaheri 2024 karibu 2025, tuache danganya toto



Pascal Mayalla

WAPENZI wasomaji wangu, tunakwenda kuumaliza mwaka 2024 keshokutwa Jumanne na Jumatano, kwa neema na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, tunauanza mwaka 2025 ambao ni mwaka wa uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani.

Hii ni makala yangu ya mwisho ya kufungia mwaka, hivyo naitumia kufanya mapitio kidogo ya mambo makubwa niliyoyazungumzia mwaka huu.

Katika mambo hayo, tunajikumbusha na kufanya mapitio niliandika kuhusu nini, nini kimefanyika na matokeo yake ni nini.

Kwa vile hii ni makala ya 52, siwezi kuyasema yote kwa kuwa nimekuwa nikiangazia masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Nimeamua kujikita kwenye masuala ya kisiasa ambayo ndiyo yanabeba mustakabali mkubwa zaidi wa amani ya nchi yetu kuelekea uchaguzi mkuu wa 2025 ili uwe huru na wa haki kwa mustakabali mwema wa taifa letu.

Kwa vile nilipoanza kazi ya uandishi wa habari mwaka 1990, Tanzania tulikuwa na magazeti mawili ya kila siku, 'Daily News' na Uhuru, magazeti matatu ya wikiendi, yaani 'Sunday News', Mzalendo na Mfanyakazi, na tulikuwa na redio moja tu, Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) na hatukuwa na Televisheni kwa Tanzania Bara lakini wenzetu kule Zanzibar walikuwa nayo. Kila kilichokuwa kinaandikwa kwenye magazeti au kutangazwa RTD, kinamfikia Mkuu wa Nchi na vya kufanyiwa kazi vinafanyiwa kazi.

Enzi hizo waandishi wa habari na watangazaji tulikuwa watu muhimu, tukiheshimika sana.

Tena mimi nikiwa mtangazaji wa RTD vipindi vya burudani, ukienda kwenye kumbi za starehe hulipi kiingilio na ukitajwa tu jina, tuko na fulani, bia za bure zinaminika kutoka kila kona, huku ukizongwa na mashabiki bila kuwasahau wale dada zetu.

Sasa hivi tuna magazeti yasiyo na idadi, vituo vya redio, TV na mitandao ya kijamii ndiyo usiseme. Sasa kila mtu ni mwandishi wa habari, kila mtu ni mtangazaji.

Hata sina uhakika kama haya tunayoandika siku hizi kwenye makala zetu, yanafika kule kunako, kwenye mamlaka husika, hivyo kujiuliza kuendelea kuandika ni kuwaandikia au kujiandikia tu?

Jambo kubwa kuliko yote nililoandika sana katika miaka hii yote minne ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhusu haki, haki, haki. Kuanzia haki katiba, haki siasa, haki uchaguzi hadi haki jinai. Kwenye maeneo hayo ya haki, serikali ya Awamu ya Sita imegusa hapa na pale lakini bado. Kubwa kuliko yote ni la haki katiba. Hilo waswahili wanasema ameliwekea pamba masikioni!

Kwa upande wa hakijinai, mnyonge myongeni haki yake mpeni. Rais Samia alianza vizuri, apewe tu maua yake. Alizifuta kesi zote za uonevu na kuwaachia huru watuhumiwa wengi, tena alitembea, kwa kizungu tunasema 'extra miles' kwa kuzifuta hata kesi zingine zenye ushahidi wa jinai kama kesi iliyokuwa ikimkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe. Ni hapa juzi kati wasiojulikana wameibuka tena na kutaka kumharibia.

Kwenye haki siasa, Rais Samia kupitia falsafa yake ya 4R, aliunda kikosi kazi kilichoongozwa na msomi nguli wa sayansi ya siasa, Prof. Rwekaza Mukandala. Wakakusanya maoni ya wadau na matokeo ya kikosi kazi hicho, aliruhusu mikutano ya siasa, akaleta sheria mpya ya uchaguzi, akabadili jina la Tume ya Taifa a Uchaguzi kuwa Tume Huru ya Uchaguzi.

Hayo mambo makubwa na mazuri yote aliyoyafanya yamekuwa kazi bure kama lile kubwa la mabadiliko madogo ya katiba kurejesha haki kuu za msingi hayajafanyika.

Watanzania tulitaka Tume Huru na Shirikishi ya Uchaguzi, Rais Samia katubadilishia tu jina.

Japo hili ni jambo jema na niliandika kupongeza lakini Watanzania walichotaka si mabadiliko ya jina wakati tume bado ni ile ile, watu ni wale wale, na tena kitu cha ajabu kabisa, muswada wa sheria ya uchaguzi uliposomwa kwa mara ya kwanza, ulifuta sheria ya uchaguzi ya serikali za mitaa.

Uchaguzi wote ulikuwa ufanywe kwa sheria moja mpya ya uchaguzi na kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi. Sijui tikitaka gani zilitembea hapo katikati, mara tukafanya uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sheria ya zamani ukisimamiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na madudu yale yale ya uchaguzi wa 2019 yakajirudia. Hapa tumefanyiwa kitu kinachoitwa Danganya Toto.

Sheria ya uchaguzi iliyokuwapo kabla ya sheria mpya, ilikuwa batili inayokwenda kinyume cha Ibara ya 5 na Ibara ya 21 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yenye haki mbili kuu za msingi- haki ya kuchagua na haki ya kuchaguliwa, zilizoporwa na Ibara ya 37 na Ibara ya 63 zilizochomekewa kiubatili ndani ya Katiba yetu.

Nilitaraji, kwa vile tumepata fursa ya kubadili sheria, hivyo tungeanza kwanza na kufanya mabadiliko madogo ya Katiba yetu, kuondoa kwanza ubatili wa Katiba kwa kurejesha haki, kisha ndipo twende na sheria yetu hii mpya ya uchaguzi. Kinyume chake, tumetunga sheria mpya ya uchaguzi yenye ubatili ule ule uliobatilishwa na Mahakama Kuu, hivyo hii sheria mpya ya uchaguzi nayo pia ni danganya toto.

Mwaka 2025, Rais Samia anayo fursa kufanya mabadiliko madogo ya Katiba, kuunda tume huru na shirikishi ya uchaguzi, kurekebisha sheria ya uchaguzi na tukafanya uchaguzi huru na wa haki.

**Kwaheri 2024, Karibu 2025 Heri ya Mwaka Mpya 2025.**
**Paskali**
**0784 270403**

KONA YA AFYA

# UGONJWA WA UVIMBE KWENYE VIA VYA UZAZI



Na Dk. Mabula Budodi

KATIKA Makala hii, tutajifunza kuhusu tatizo ambalo limekuwa linasumbua watu wa jinsia ya kike wakiwa katika umri wa kupata ujauzito. Ni ugonjwa ambao huwapata watu kuanzia wanapovunja ungo mpaka ukomo wa hedhi.

Neno PID kwa Kiingereza lina maana ya 'pelvic inflammatory disease' kama wengi wanavyokutana nalo katika nyanja za afya likitumiwa mara nyingi ili kurahisisha uelewa na kwenye makala hii, tutapata ufahamu zaidi juu ya jambo hili.

**PID NI NINI?**

Ugonjwa huu umekuwa sababu kubwa ya matembeleo ya madaktari katika sekta ya afya kwa wakati huu kutokana na kuwa na dalili za kukera sana kwa mwanamke. Wengi pia hufika kwa madaktari wakiwa wameshachelewa sana kutokana na kuwa na uelewa hafifu juu au kuwa na aibu huhusu suala hili.

PID ni ugonjwa wa uvimbe kwenye via vya uzazi au wakati mwingine huitwa 'fupanyonga'. Ni ugonjwa ambao husababishwa na bakteria wanaonzia kwenye uke wa mwanamke na kupanda sehemu ya juu ya uzazi ya mwanamke ikihusisha maambukizi ya kwenye njia au shingo ya uzazi, mirija ya mfuko wa uzazi kitaalamu falopio, mayai yaani ovari na hata ukuta wa mji wa uzazi, yaani 'uterace' kwa kitaalamu.

**SABABU ZA KUPATA PID**

Ugonjwa huu wa fupanyonga umeonekana ukisababishwa zaidi na bakteria kama ilivyoelezwa awali. Bakteria hawa ni pamoja na kisonono na klamidia wameonekana wakihusika karibu asilimia 85 na asilimia 15 iliyobaki imekuwa ikichangiwa na vitu vingine au bakteria wengine tofauti.

Bakteria wanaosababisha ugonjwa wa kisonono na klamidia wanaambukizwa kwa njia ya kuambukizana au ngono, hivyo huweza kusambazwa kwa namna hiyo kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine.

Watu walio katika hatari zaidi ya kupata ugonjwa huu ni pamoja na wanaoanza kufanya ngono katika umri mdogo, yaani chini ya miaka 25 kwa sababu imeonekana zaidi watu wa umri wa miaka 15 na 35 huathirika zaidi.

Kuwa na maambukizi ya magonjwa ya zinaa kama kisonono na klamidia, kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja, kuwa na historia ya kuwa na ugonjwa huu wa fupanyonga, kuharibika au kutoka kwa mimba, kusafisha kwenye mji wa uzazi baada ya mimba kuaribika au kwa sababu nyingine ya kitaalamu yeyote ile, kupiga bomba(kusafisha kwa kuogesha kwa kutumia sabuni kuingia hadi ndani kabisa ya uke wa mwanamke.

**DALILI ZA MWENYE PID**

Dalili za mtu mwenye PID ni nyingi na ni tofauti tofauti lakini muda mwingine, mtu huweza kufikwa na dalili chache sana au kutowa na dalili yoyote isipokuwa na shida ya kupata mtoto tu.

Dalili hizi huweza kuonekana zaidi baada ya kumaliza hedhi au siku chache baadaye au muda mwingine viashiria hutokea kuonekana wakati wa hedhi.

Dalili hizi za fupanyonga ni pamoja na kutokwa uchafu kwenye via vya uzazi. Uchafu unaomtoka mwanamke huwa si wa kawaida kwa kuwa na harufu kali au kubadilika rangi isiyokuwa ya kawaida.

Hii inamaanisha kwamba uchafu unaomtoka mwanamke kuwa mzito kama maziwa ya mgando ambao huweza kuashiria maambukizi ya fangasi za uke, kuwa wa kahawia, kijani au njano. Uchafu wa mwanamke hautakiwi kuwa hivyo bali inabidi usiwe na rangi, mwepesi wala harufu.

Dalili nyingine huweza kuwa maumivu ya chini ya tumbo la uzazi, maumivu makali sana wakati wa tendo la ndoa, maumivu wakati wa haja ndogo, kutoka damu wakati wa tendo la ndoa, na kuwa na hedhi zisizoeleweka, yaani kutokuwa na mpangilio.

Kutokana na kuwa na dalili tofauti kwa wanawake, mara nyingi utambuzi wa kuwa na ugonjwa huu umekuwa hafifu mpaka pale mwanamke anapopatwa na dalili mbaya zaidi, hivyo kwenda hospitalini.

**UTAMBUZI WA UGONJWA**

Utambuzi wa ugonjwa wa fupanyonga huhusisha kuonana na daktari atakayekusikiliza dalili zako, kufanya vipimo katika via vya uzazi, kupima uchafu unaotoka katika mji wa uzazi, kuangalia bakteria wanaoweza kusababisha ugonjwa huu, kufanya picha ya tumbo na kuangalia madhara mengine yanayoweza kusababishwa na ugonjwa huu.

**MATIBABU YAKE**

Matibabu ya jambo hili huweza kuhusisha kuanzishiwa dawa za antibiotiki za kumeza au kuchoma kutokana na ukubwa wa tatizo hata za kuingiza katika uzazi ili kusaidia kuondoa uchafu unaotoka katika njia hiyo.

NAMNA YA KUZUIA

Kuzuia maambukizi ya fupanyonga kunaweza kufanyika kwa kuepuka ngono zembe, kuacha kuwa na wapenzi wengi, kuwa na elimu juu ya ugonjwa huu, kusafisha pale inapotoka mimba katika hospitali na kutumia antibiotiki baada ya kuzuia na kutibiwa magonjwa ya zinaa yanapojitokeza na kufanya uchunguzi wa mara kwa mara juu ya magonjwa ya zinaa.

**MADHARA YA PID**

Madhara ya PID ni pamoja na maumivu makali sana ya tumbo la uzazi, kupata ugumba, yaani kupunguza uwezo wa kukamata mimba hata wakati mwingine mimba kutunga nje ya mfuko wa uzazi jambo ambalo ni hatari zaidi pale inapopasuka.

Ni muhimu zaidi kutibiwa na kuzuia maambukizi ya mara kwa mara ya ugonjwa huu. Kwa maelezo zaidi, onana na daktari wako na kupima afya mara kwa mara kujua kama una maambukizi ya PID.

**-Dk. Budodi ni daktari wa binadamu anapatikana Dar es Salaam. Kwa maelezo na ushauri zaidi kuhusu afya, wasiliana naye kwa simu 0710 980076 au baruapepe mabulabudodi@gmail.com**

# HABARI PICHANI



Mchuuzi wa mito ya kulalia, akitafuta wateja katika barabara ya Bamaga jijini Dar es Salaam ambapo mto mmoja unauzwa kwa shilingi 10,000.




Msukuma mkokoteni akiwa amepakia mzigo mkubwa huku akiwa hana mtu wa kumsaidia kusukuma katika Soko la Tandale Dar es Salaam jana.



Abiria akiwa amepanda juu ya baiskeli ya miguu mitatu (guta), bila kujali usalama wake huku guta hilo likiwa limepakia mzigo wa viazi na nyanya Manzese Dar es Salaam jana.



Mteja akichagua viatu vilivyopangwa kandokando ya barabara ya Morogoro, Manzese jijini Dar es Salaam ambapo pea moja inauzwa kwa shilingi 5,000 jana.



Mjasiriamali akiwa amebeba bidhaa zake akitafuta wateja katika eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam jana.




Mkuu wa Mikakati na Uendelevu wa Benki ya NCBA , Charles Mbatia, akiumwagia maji mti aliopanda katika Shule ya Sekondari Jangwani ambapo benki hiyo imetoa miti 1000 katika shule hiyo kwa ajili ya utunzaji wa mazingira shuleni hapo jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**

MAISHA
DESEMBA 29, 2024
Nipashe
Baba, Mama na ... Jumapili

NYUMBA
Ukurasa 15



Boresha nyumba yako mara kwa mara





# FURAHIA 'NECK VEST'


Ukurasa 13

## WATOTO

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








### FUMBO TOTO

Wiki hii tumerudi katika anga za Jiografia, badilisha miji hii kuwa nchi kisha ujaze katika vyumba vilivyo wazi.


ROME, LOME, TRIPOLI, BAMAKO, NEW DELHI, LIBREVILLE



### TOA TOFAUTI 5



### PAKA RANGI





### AMSHA AKILI

RAFIKI YETU AMEPIGWA JIWE... JE, ANASEMA NINI? FUTA HERUFI YA KWANZA, KISHA ACHA INAYOFATA, FUTA TENA INAYOFATA... FANYA KWA KILA HERUFI MPAKA MWISHO.




### CHEKA



**Alichokifanya daktari**

Msikie mtoto huyu akimuuliza maswali baba yake.

**Mtoto:** Baba unaweza kumwachia hilo gari lako dada wa kazi akaliendesha?

**Baba:** Siwezi kumwachia gari langu hili aliendeshe ni ghali sana.

**Mtoto:** Je, mnaweza kumwachia chumba chenu dada wa kazi kikiwa wazi na mkaenda kazini?

**Baba:** Haiwezekani kamwe, kuna vitu vya gharama na pia heshima haitakuwepo.

**Mtoto:** unaweza ukampa dada kadi ya ATM yako na namba ya siri ukakuchukulie pesa?

**Baba:** Mtoto una balaa wewe, unataka siku akiiba hii kadi akachukue pesa zote tuwe maskini, sithubutu.

**Mtoto:** aahaaaaaa, kumbe hauwezi kumkabidhi chochote chenye thamani dada wa kazi, sasa kwa nini mnanikabidhi mimi kwake nyie mnaenda kazini mpaka mnarudi, kumbe mimi sina thamani kwenu eeeeh

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mwanamume simama kwenye nafasi yako ndoa ipone!

KARIBU msomaji wangu tuuage mwaka 2024 na tupeane Heri ya Mwaka Mpya 2025. Tunapouaga mwaka 2024, ni muhimu tutafakari miongozo itakayolinda familia zetu mwaka mpya.

Huko nyuma nimejadili sana masuala yanayohusiana na ndoa. Leo naomba nimulike wanaume juu ya mambo ya msingi wanayopaswa kuzingatia kwenye nafasi zao kama baba wa familia.

Kuna kitu kikubwa sana Mungu anatarajia kwa kinababa. Mungu anawathamini, hivyo msimwangushe. Mungu alimwumba mwanamume kwa kumwamini. Alimpa nafasi ya kwanza kupokea pumzi!

Hiyo ilikuwa nafasi ya kipekee kwa mwanamume. Hata siku moja usijute eti kwa nini Mungu alikuumba mwanamume. Alipokuumba na kukuweka tumboni mwa mwanamke alikuthamini.

Mwanamume ni kichwa, aliumbwa kwanza na kuona ni kitu chema. Na alipoumbwa alipewa kazi, si ajira. Kila mwanadamu aliumbwa akiwa na vitu vyote siyo nusu nusu.

Mungu alimwumba mwanamume kipekee, ni kichwa na msingi akichanganyikiwa familia lazima iyumbe. Aliumbwa kwa kusudi, kwa kazi maalumu. Ili mwanamume awe mwanamume, atatambulika kwa kazi au majukumu yake.

Mwanamume usioe kabla ya kazi. Mwanzo 2:15 inasema: “BWANA, Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza.” Hapa inadhihirisha kwamba Mungu alimwumba mwanamume na kumpa kazi kabla ya kumpa mwanamke.

Kwa mantiki hiyo, aliyepewa kazi na maelekezo toka kwa Mungu ni mwanaume. Hivyo, kilichoanza kwanza ni kazi kwa Adamu, kisha Mungu akamwumba mwanamke kama msaidizi wake.

Mwanamume alipewa maelekezo usile mti huu. Kama mwanamume angetii maelekezo, mwanamke asingebabaika. Kwa maana nyingine, Adamu hakusimama kwenye nafasi yake.

Kama nilivyoeleza hapo awali, mwanamume ni mwakilishi wa kwanza wa Mungu na anapofeli, anamfanya Mungu hana nguvu. Leo tupo hapa tulipo kutokana na babu au baba zetu hawakutambua kazi yao ni nini hapa duniani.

Mwanamume lazima aelewe kuwa yeye ni taa/nuru. Na kwamba nafasi ya mwanamume aliyejitambua inabaki pale pale, mwakilishi wa Mungu.

Mwanamke yeye aliumbwa kutoka katika ubavu wa mwanamume, akafananishwa na msaidizi kufanikisha maono ya mwanamume. Aliletwa kuongozwa, kuelekezwa. Ni ukweli usiopingika kwamba amepewa uwezo mara mbili. Mwanamke ukimpa mwongozo anaweza kufanya maradufu.

Shetani akitaka kuua ulimwengu humvaa mwanamume kwa kwa kuwa anajua vyema uwezo wa mwanamume. Anachofanya ni kupenyeza mawazo kudhoofisha wanaume.

Ili mwanaume ambaye ni mwakilishi wa Mungu asiangushwe na maadui, yako mambo kadhaa ya msingi ambayo anapaswa kuyazingatia na kuyasimamia.

Kwanza, mwanamume lazima awe mstari wa mbele kwa mambo ya Mungu. Hapaswi kuwa mbali na Mungu. Huwezi kuongoza familia yako bila Mungu, utakuwa unajidanganya.

Ukimtafuta Mungu, familia yako itakuwa rahisi kumjua Mungu. Kuwa na imani na Mungu, mwamini Mungu ndivyo utakavyofanikiwa.

Mwanamume anatumia akili, anaongozwa na akili. Hata hivyo, Mungu anasema tumtumaini Yeye kwa moyo wote wala tusizitegemee akili zetu wenyewe. Hakikisha imani yako unaiweka kwa Mungu.

Pili, fanya kazi kwa bidii mwanaume. Kabla ya mwanamke Mungu alikupa kazi. Tambua kazi yako uifanye kwani si tu kiongozi wa familia, taifa pia linakutegemea.

Mwanamume akivurugwa utaona na mwanamke anakuja juu kwa kuwa hakuumbwa na jeuri, ni mpokeaji si mtoaji! Na mwanamke unachompa anakizalisha mara mbili.

Ndoa nyingi zimekufa kwa sababu nyingi. Ni kosa kuruhusu mwanamke ajiongoze. Ana ufahamu zaidi. Kama kusoma kwa bidii ni mwanamume anapaswa kusoma, asijiwekee mipaka.

Mwanamume anapaswa kujifunza jinsi ya kuishi na mwanamke. Kwa mfano, wako wanawake viongozi kwa asili. Chimbuko lao ni uongozi na kwao wengi ni viongozi. Kama mwanamume hutajipanga kujua jinsi ya kumtumia, utafeli!

Kabla hujaoa usiangalie mwonekano wa nje sura au umbo. Usioe tu kwa mhemuko, hisia eti ni mwimbaji. Kwenye ndoa hakuna kuimba. Kabla ya kuoa tengeneza msingi wa mahusiano.

Mwanamume ukioa kiongozi lazima ujue, vinginevyo utajishangaa. Ukioa kabla hujamsoma utajikuta unachepuka. Jifunze kumsoma mtu, je, ni mwanamke wa aina gani? Wanawake wengi tumekuwa chanzo cha wanaume kuathirika ndani ya ndoa!

Jambo lingine ambalo limekuwa mwiba kwa wanaume wengi ni kulishwa na wanawake. Mwanamume usikubali kulishwa na mwanamke, atakudharau. Pia mwanamume akiomba heshima kwa mwanamke, hiyo ni shida. Heshima haiombwi.

***Wiki ijayo nitaendelea nini mwanamume afanye ili asimwangushe Mungu. Maoni 0715268581. Namba pia iko WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Kumbe kiburi ni aina nyingine ya ukatili?

MAJIVUNO ambayo hayajashughulikiwa, huanza kuunda mtazamo mbaya juu ya maisha ambao huzingatia hasi badala ya chanya.

Sisi ni wepesi wa kuwahukumu wengine kwa kasoro zao huku tukipuuza ukweli kwamba sisi pia tuna kasoro. Maisha yetu yanaanza kuingiwa na ushindani badala ya umoja.

Kwahiyo anza kutafakari na usiache kiburi kikakuharibu. Hicho kiburi ulicho nacho kinaweza kutokana na umaarufu ulio nao, utajiri, ubaguzi wa jamii, tofauti ya tabaka na jamii, elimu, sifa na mamlaka.

Kwa njia tofauti, kiburi kinaweza kukuingia kwa urahisi na kiharibu utu wako.

Watu wengi huonekana kuwa wanyenyekevu wanaposhughulika na wakuu wao au hata watu wa rika lao. Lakini ni nini hutokea wakati anayeonekana kuwa mtu mnyenyekevu apatapo cheo cha mamlaka?

Hata wafanyakazi wa serikali wanaweza kuwa na kiburi wanaposhughulika na umma, wakifikiri kwamba umma wapaswa kuwatumikia badala ya wao kuutumikia.

Ndugu yangu, kiburi chako kinaweza kukufanya uwe mkali, bila hisia, unyenyekevu unaweza kukufanya uwe mwenye fadhili.

Wiki hii nimemsikia Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo, akilizungumzia jambo hili kwa ufupi, ndiyo maana leo nikaamua kujikita kulifafanua katika muktadha huo.

Askofu Shoo, yeye aliwasihi Watanzania kuwaondoa kwenye moyo wao wapangaji wabaya, akihadharisha hata ukiwa na mali nyingi na maarifa mengi, kama wako wapangaji hao ni kazi bure.

Alisema matokeo yake si furaha bali ni kuishia kwenye uchungu, kukata tamaa na kuchukiana.

Askofu Dk. Shoo alisema: “Toa wapangaji wabaya moyoni mwako, ambao wanamzuia Yesu asiingie na asiwe na nafasi katika maisha yako yote. Iwe ni kiburi, iwe ni majivuno, iwe ni uchoyo, iwe ni ubinafsi, iwe ni tabia mbaya za kumchukiza Mungu. Hawa ni wapangaji wabaya umewaweka katika moyo wako.

“Siku zote huwa kuna maneno ya kumalizia yasiyojenga. Ndiyo, huenda hilo likawa kweli, lakini ana tatizo hili au kasoro ile.

“Inawezekana hata kukosa imani ya kweli kwa Mungu umuaminie. Mali nyingi, maarifa mengi, kama umeweka wapangaji wabaya inakuwa ni kazi bure. Matokeo yake ni si furaha, ni kuishia kwenye uchungu, kugombana, kukata tamaa na kuchukiana. Haya yote tunayokumbatia hatma yake ni uchungu na kuangamia.”

Sasa swali la kujiuliza hapa, ni je, wewe umewahi kushughulika na mtu aliyejaribu kimakusudi kukufanya uhisi kuwa mtu asiye wa maana?

Labda meneja, msimamizi, mwangalizi au hata mtu wa jamaa aliyekuona kuwa duni na kukudharau kabisa?

Ulihisije kuhusu mtu huyo? Je, ulivutiwa na utu wake? Hata kidogo! Kwa nini? Kwa sababu kiburi huleta vizuizi na hukomesha mawasiliano.

Kiburi humfanya mtu adharau kila mtu ili yeye siku zote aonekane kuwa bora zaidi. Mtu aliye na mtazamo kama huo, mara nyingi hasemi neno zuri kuhusu wengine.

Siku zote huwa kuna maneno ya kumalizia yasiyojenga. Ndiyo, huenda hilo likawa kweli, lakini ana tatizo hili au kasoro ile.

Katika kitabu ‘Thoughts of Gold in Words of Silver’, kiburi kinaelezwa kuwa ni uovu wenye kushinda siku zote.

Kwa kweli, matokeo ya kiburi mara nyingi, ni kukosa marafiki wa kweli na kinyume cha hilo, ulimwengu hupenda wanyenyekevu.

Si wanyenyekevu ambao wana fahari ya kuwa hivyo, bali wanyenyekevu kikweli. Hata maandiko matakatifu katika Biblia yanasema, kiburi cha mtu humletea aibu, yeye ajinyenyekezaye atapata heshima.

Kiburi hutangulia uangamivu na roho yenye kutakabari hutangulia maanguko. Afadhali kuwa na roho ya unyenyekevu pamoja na maskini, kuliko kiburi.

Kifupi ni kwamba, dharau au majivuno humfanya mtu akanyage kanyage mioyo ya wenzake. Naam, mtu mwenye kiburi anaweza kujiona, kuwa mfidhuli, mwenye kuwaaibisha wengine.

Yeye hufurahia kumwumiza kwa njia yenye ubaridi, isiyo na hisia, kisha huchekelea hali mbaya na ya kufedhehesha ya yule mtu mwingine. Lakini kushusha au kuharibu staha ya mtu mwingine, ni upanga ukatao kuwili. Husababisha kumpoteza rafiki na hata yaelekea sana, kumfanya awe adui.

Nawatakia Heri ya Mwaka Mpya wa 2025 na baraka za Mwenyezi Mungu katika kazi halali za miki=ono yenu.

• ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI



**ILIKUWA** siku ya furaha kwa familia ya Tunu Hassan ambaye ni mtangazaji wa EFM Radio baada ya kumuandalia sherehe ya kumuaga kabla ya kufunga ndoa. Sherehe hiyo ilifanyika Desemba 19, mwaka huu katika ukumbi wa Suma JKT Mwenge, Dar Es Salaam.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

## FURAHIA 'NECK VEST'

VAZI la Vesti limekuwa maarufu kwa watu wa aina zote, lakini kuna toleo jipya linalofahamika kama 'Neck Vest' maalum kwa wanawake.

Nguo hizi zimetengenezwa kutokana na mchanganyiko wa nailoni na pamba.

Vesti za aina hii huwa laini, yenye mwonekano wa kipekee na inayovutika.

Vazi hili halifai kutumika katika shughuli za umma, linapendeza zaidi katika matembezi ya jioni au karamu na hafla za nje.

Inapendeza zaidi endapo utakuwa na chaguo zuri la rangi, unashauriwa kununua ya rangi nyeupe, kijivu na nyeusi.

Ukitaka kupendeza zaidi unaweza kuvaa ndani nguo nyingine kama shati, fulana au prova.





## UREMBO

Na Mary Geofrey

# Kinywa kinacholeta furaha

TATIZO la kunuka kinywa husababisha mtu akose furaha na kupata msongo wa mawazo baada ya kutengwa na jamii.

Mtu mwenye matatizo hayo huweza kuharibu mahusiano na mwenza au watu wake wa karibu.

Bahati mbaya Watanzania wengi wenye tatizo la kunuka mdomo hawajitambui mpaka aambiwe na mtu wake wa karibu tena mwenye upendo na anaye jiamini.

Kwa bahati mbaya sana tatizo la kunuka mdomo kwa wanawake huwaondolea uwezo wao wa kujiamini na kujiona siyo warembo katikati ya wanawake wengine.

Kuna njia kadhaa za kutumia kumaliza tatizo hili ni muhimu tukazifuata.

**SAFISHA ULIMI VIZURI**

Watu wachache sana huchukua zaidi ya nusu dakika kusafisha ulimi, siri ni kwamba ulimi unatunza sana uchafu katika kinywa, hivyo kuepuka harufu mbaya safisha ulimi vizuri.

Unaweza tumia kijiko kutoa uchafu au nunua 'tongue cleaner' kwa bei nafuu kwenye maduka ya dawa. Tuwafundishe watoto tabia hii mapema.

**KISAFISHA KINYWA**

Njia nyingine rahisi ya kupata harufu nzuri au fresh breath ni kutumia maji ya chumvi kusuuza mdomo wako. Ni rahisi, haina gharama na haina madhara. Weka chumvi kwa glass ya maji sukutua .Ukiweza kununua mouthwash za dukani kama listerin ni vizuri pia.

**MDALASINI NA HILIKI**

Hivi viungo vinatumika toka kale na wahenga kuweka harufu nzuri mdomoni.Ukila vyakula vyenye viungo vingi au ukihisi mdomo haueleweki chukua punje ya hiriki au kipande cha mdalasini tafuna.Ukiweza chemsha maji ya viungo hivi na sukutua.

**TUFAA, TANGO, PERA**

Matunda kama haya yanaongeza mate mdomoni na kuzuia uwepo wa bakteria ambao husababisha harufu mbaya. Kula kipande cha tango au apple hasa baada ya chakula. Pera husaidia wale wanaotoka damu kwenye fizi pia.







## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Utamu wa uji wa ngano



UJI wa ngano ni miongoni mwa vyakula vya lishe wanavyotakiwa kula watu.

Chakula hiki huandaliwa kwa kutumia ngano isiyokobolewa ambayo inasifika kwa wingi wa virutubisho kama vitamini B, vitamini E, madini chuma, shaba, zinki, magnesiamu, kemikali asilia za mimea na nyuzi nyingi ambazo husaidia katika mmeng'enyo wa chakula.

**Mahitaji**

Ngano nusu, sukari robo, chumvi kijiko kimoja cha chai, maziwa lita moja, maji glasi tatu na hiliki kiasi.

**Namna ya kupika**

Hatua ya kwanza ni kuloweka ngano katika maji kwa saa 3 mpaka 5 ili kuifanya ngano kuwa laini kabla ya kupika, kama huwezi kuloweka ngano unaweza kuisaga kidogo katika blenda ili upate mchanganyiko wenye unga.

Baada ya hapo bandika sufuria jikoni changanya maji na unga wa ngano nzima kisha upike kwa moto wa wastani huku ukikoroga mara kwa mara ili kuzuia kushikana au kushika chini ya sufuria.

Ongeza chumvi na sukari kama unataka na endelea kupika kwa dakika 10-15 kisha uweke viungo kulingana na uhitaji wa walaji.

Baada ya hapo weka tui la nazi au maziwa (tumia kimoja wapo) kisha punguza moto na uache uji uchemke kwa dakika nyingine 5-10 ili kuhakikisha ngano imeiva vizuri.

Hatua ya mwisho ni kuepua uji na kuacha upoe kidogo kabla ya kutenga na watu wanywe.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Boresha nyumba yako mara kwa mara

MABORESHO ya nyumba yanapaswa kufanyika mara kwa mara katika kuimarisha ustawi wake.

Mbali na kufanya maboresho kwa ajili ya kuiimarisha, pia kunachangia kwa kiwango kikubwa iendelee kuwa na mvuto. Nyumba ambayo hufanyiwa matengenezo au kuboreshwa mara kwa mara, hudumu kwa muda mrefu tofauti na ile ambayo haijafanyiwa maboresho.

Kutokana na ukweli huo, ndiyo maana kumekuwa na msisitizo wa kuwapo kwa utamaduni wa kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya nyumba. Kuna muda maalum ambao hushauriwa kufanya matengenezo au maboresho ya nyumba baada ya kumaliza ujenzi na kuanza kuishi.

Msanifu Majengo, Amos Kuvilo, anasema kuna umuhimu mkubwa wa kutofautisha uso wa mbele wa nyumba na maeneo mengine ya nyumba hiyo.

"Kuna nyumba zingine zimekosa mwonekano mzuri wa mbele,hivyo husababisha kushindwa kutofautisha uso wa mbele na wa nyuma wa nyumba au upande wa kulia na kushoto. Hapa ndipo tunasema kwamba kuna haja kwa msanifu kutumia maarifa kuandaa ramani ambayo itakidhi mahitaji ya nyumba husika,"anasema Kuvilo.

"Baadhi ya sehemu za mbele za uso wa nyumba ambazo ni muhimu kuzipendezesha ni nguzo ambayo ni sehemu ya jengo iwe ya duara, mstatili au mraba. Hii itategemea namna ilivyosanifiwa, lakini cha msingi ni kuhakikisha inatengenezwa kwa ustadi mkubwa," anasisitiza.

Pia anasema katika kutengeneza uso wa mbele wa nyumba, ni vizuri kutumia malighafi ambayo ni rafiki wa mvuto wa macho, imara na ambayo haina madhara kwa binadamu.

"Hili linawezekana kwa sababu Wasanifu wanafahamu malighafi bora za kutumia katika kutengeneza eneo hili kwa hiyo ni vema kuwatumia ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima,"anasema Kuvilo.

Mbali na nguzo, anasema madirisha nayo ni eneo muhimu ambalo linapaswa kuwekewa urembo hususani lililoko mbele ya uso wa nyumba.

"Na katika kutengeneza dirisha la mbele la uso wa nyumba, hapa napo kutategemea na vigezo vya sehemu au sababu za kisanifu, Msanifu anatakiwa kutumia utaalam wake kupendekeza aina ya dirisha kulingana na malighafi anayotaka kuweka iwe ni kwa mlalo au unyoofu," anasema.

Eneo lingine la kuboresha kwenye uso wa nyumba ni milango ya nje.

Anasema milango ya nje bila kujali aina zake, hutumiwa kwa kuzingatia aina ya mtiririko wa kisanifu ili kutokupoteza mnyororo mzima wa mtindo na mpangilio wa jengo ulivyo.


Kuvilo anashuri kwamba wakati maboresho au matengenezo yanafanywa kwa ajili ya kupendezesha uso wa mbele wa nyumba, ni vema kutokusahau na uchaguzi wa rangi kwenye ukutwa na dizaini katika valanda lake katika uso huo wa mbele wa nyumba.



# 2025 unabadili mtindo kuta za sebule

WAKATI upo katika maandalizi ya kuingia mwaka mpya 2025, jambo la kipekee ni kubadili mwonekano wa kuta za sebule ili kuonekana nadhifu na wa kipekee.

'Wall paper' ni pambo linaloweza kubadili mazingira ya nyumba kwa kiwango kikubwa mno kutokana na aina ya picha zinazotengenezwa kupata aina hiyo ya pambo.



Mwaka 2025 utaanza kwa aina mpya ya wall paper ikiwamo picha inayoonesha jua likichomoza, ambayo ukiiweka ndani unapata mandhari nzuri.

Iko picha nyingine ya fukwe ikionesha kujaa kwa maji ambayo inaleta mazingira ya utulivu wa hali ya juu.

Mandhari nyingine inayobamba kwenye aina hii ya pambo ni picha ya msitu au bustani ya maua mazuri. Pia picha inayoonesha barabara au mbuga ya wanyama.

Mtaalamu wa mapambo ya nyumbani, Brigitte Didas, anasema picha inayoonesha jua likizama inafaa ile ambayo imepigwa kwa kuchukua mazingira ya mto au maji na aina kiasi ya miti.


Anasema nyingine ni inayoonesha zaidi mawingu na hasa iliyopigwa kwa juu na mtu akiwa ndani ya ndege.

Kwa mujibu wa Brigitte, picha ya msitu inawafaa watu wanaopenda mazingira asilia na kwamba ili ikae vizuri, iwekwe mwishoni mwa korido.

"Wall paper ya hifadhi za wanyama inafaa iwe na kundi la ina moja ya wanyama kama twiga au simba kulingana na mtu anavyopenda, uzuri wa wallpaper ni kwamba ni rahisi kuitoa pale unapohitaji kufanya hivyo wakati wowote," anasema.

Anashauri kuweka aina hizi za wallpaper kwenye ukuta mdogo na hasa kwenye kona ili kuongeza ukubwa wa eneo. Pia ni picha nzuri inayoweza kuwekwa upande wa pili wa kioo.

# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRA
FIGISU FIGISU
KWA HERI 2024
KARIBU 2025
R.I.P
KASHESHE
MASHABIKI WAMEUANA KWA WAZIMU WAO!!! MIMI NILIKUWA REFA SIHUSIKI NA MAUAJI
LABDA UKAKATAE HUKUWA REFA
KITAA CHA KWETU
HIZI CHANGAMOTO ZINAZOLIANDAMA SOKA LETU MBONA SIONI JITIHADA ZA KUZITATUA?!
CHANGAMOTO ZA SOKA LETU TUKUFU "HAZITATULIWI"KAMA NGUO KWA FUNDI CHEREHANI!
MECHI ZA USIKU UNAZOKWENDAGA KUANGALIA IPO SIKU UKWELI UTABAINIKA!
USIOMBE HIYO SIKU IFIKE UPESI...UNAWEZA UKAPARARAIZI!!!
KWANI KUPANGA MATOKEO KWENYE MECHI ZA LIGI KUNASAIDIA NINI?
KUNASAIDIA KUTENGENEZA UCHOCHORO WA "KUPIGA HELA"
NDANI YA KIBASI
TULIPOFIKIA KI'SOKA NI WAZI TUNAHITAJI MUWEKEZAJI ATUSAIDIE KULISUKUMA MBELE SOKA LETU
HAPA MNASTAREHESHA SAFARI ILI TUSISINZIE... NANI ATAWEKEZA KWENYE UOZO?!
AAAAH! USISEME HIVYO! MBONA JUZIJUZI KUNA MTU KATAKA KUNUNUA KLABU KUBWA NCHINI YENYE UTANI WA JADI?
HUKUJUA NIA YAKE!
HATA MIMI NILIKUWA NAFIKIRIA KAMA WEWE! AKIPATIKANA MUWEKEZAJI TUTAKUWA KAMA ULAYA
NIA GANI ZAIDI YA KUTAKA IWE MFANO WA KUIGWA?
WAPIGAJI MTAWAELEZA LUGHA GANI IWAKOLEE?
ALITAKA KUINUNUA ILI AIWEKE KAPUNI APUMZIKE NA MIKELELE ISIYO NA TIJA
JAMANI SISI TUSHAUMBWA TUCHEZE KWETU HAPA HAPA
MPAKA HAPA MPIRA UMEKWISHA NA MSHINDI TAYARI KESHAPATIKA... AMBAYE NI SISI
KWA KIWANGO HIKI GOLI NI MALI YENU NITAWAPATIA NYONGEZA YA MABAO MANNE.
CHOBINGO HOTEL
HII MISTRESS MINGINE NI YAKUJITAKIA!!! KWANI SIWEZI KUWA MTU MPAKA NIWE SHABIKI WA MPIRA?
SIJUI NINYWE DAWA GANI NIPONE UGONJWA WA JAKA-MOYO LA USHABIKI!!!

HABARI KIMATAIFA

# Wanajeshi wa Israel wachoma moto Hospitali Ukanda wa Gaza

**GAZA,** PALESTINA

MAOFISA wa wizara ya afya Ukanda wa Gaza, wameripoti kwamba wanajeshi wa Israel walivamia na kuchoma moto moja ya hospitali iliyobaki ikitoa huduma Kaskazini mwa Gaza.

Wanajeshi hao waliichoma hospitali hiyo baada ya kuwafukuza wafanyakazi wa hospitali na wagonjwa waliokuwepo.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, moto uliteketeza maeneo kadhaa ya hospitali ya Kamal Adwan, ikiwamo maabara na idara ya upasuaji.

Jeshi la Israel lilidai kuwa hospitali hiyo ilikuwa ikitumiwa na wapiganaji wa Hamas kama kituo chao cha operesheni, lakini halikutoa ushahidi wowote kuthibitisha madai hayo.

Katika taarifa yao, jeshi hilo lilieleza kuwa kulitokea moto mdogo katika jengo tupu la hospitali lakini halikujua chanzo chake.

Tukio hilo limeongeza hali ya wasiwasi na machungu kwa wakazi wa Gaza, ambao tayari wanakabiliwa na mateso kutokana na vita vya muda mrefu.

Ripoti kutoka Wizara ya Afya ya Gaza, zinaonesha kuwa zaidi ya Wapalestina 45,400 wameuawa tangu kuanza kwa vita vya Israel dhidi ya Hamas.

Zaidi ya nusu ya vifo hivi ni wanawake na watoto, hali inayoongezidisha machungu katika jamii ya Wapalestina.

Vita hivyo vilianzishwa na Hamas Oktoba 7, 2023, baada ya kufanya shambulio kusini mwa Israel ambalo liliua watu takriban 1,200 na kuwachukuwa mateka watu 250.

Hadi sasa, mateka 100 bado wanashikiliwa Ukanda wa Gaza, ingawa ni theluthi mbili ya mateka wanaaminika kuwa hai.

Hali hiyo imezidi kuibua maswali kuhusu mustakabali wa ukanda huo na mateso yanayoendelea.

Familia nyingi zilizokimbia makazi yao zinakabiliana na hali mbaya ya maisha wakati wa msimu wa baridi. Katika kambi za muda kando ya ufukwe wa bahari wa Deir al-Balah.

Licha ya baridi kuwa kali, Wapalestina wanalala kwenye mahema yaliyojengwa kwa maturubai na vitambaa vilivyoshikiliwa kwa kamba na mbao, ambayo hayana ulinzi wa kutosha dhidi ya upepo mkali kutoka baharini.

Muhammad al-Sous, ambaye anaishi katika kambi hiyo, alieleza kuwa watoto wake wanakusanya chupa za plastiki kwa ajili ya kuzichoma ili kupata joto.

**DW**

# Trump aomba kucheleweshwa hukumu TikTok

**NEWYORK,** MAREKANI

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, ameiomba Mahakama ya Juu kucheleweesha hukumu yake ya kupiga marufuku mtandao wa TikTok wa China.

Wakili wake aliwasilisha ombi la kisheria mahakamani juzi, ambalo linaeleza kwamba Trump anapinga kusitishwa kwa mtandao wa TikTok na anatafuta njia ya kutatua suala hilo kisiasa mara atakapoingia madarakani.

Januari 10, mahakama hiyo inatazamiwa kusikiliza hoja kuhusu sheria ya Marekani inayomtaka mmiliki wa TikTok raia wa China, ByteDance, kuiuza kampuni hiyo ya mitandao ya kijamii kwa kampuni ya Kimarekani la sivyo atapigwa marufuku ifikapo Januari 19, siku moja kabla ya Trump kuchukua madaraka.

Maofisa wa Marekani na wabunge walikuwa wameshutumu ByteDance kwa kuhusishwa na serikali ya China, jambo ambalo kampuni hiyo inakanusha.

Madai hayo ya programu ambayo ina watumiaji milioni 170 nchini Marekani yalisababisha Bunge la Congress kupitisha mswada mwezi Aprili, ambao Rais Joe Biden alitia saini kuwa sheria, moja ya sharti ni kupiga marufuku.

TikTok na ByteDance waliwasilisha changamoto nyingi za kisheria dhidi ya sheria hiyo, wakisema kwamba inatishia ulinzi wa uhuru wa kujieleza wa Marekani.

Kwa kuwa hakuna mnunuzi aliyepatikana kufikia sasa, nafasi ya mwisho ya kampuni hiyo kuzuia kusitisha huduma yake ni kupitia mahakama kuu ya Marekani.

Ingawa Mahakama ya Juu hapo awali ilikataa kufanyia kazi ombi la zuio la dharura dhidi ya sheria hiyo, ilikubali kuruhusu TikTok, ByteDance na serikali ya Marekani kusikiliza kesi zao Januari 10.

**BBC**




Madaktari wakiwahamisha wagonjwa waliojeruhiwa na wa saratani kutoka Hospitali ya Kamal Adwan katika eneo la Beit Lahia, kaskazini mwa Ukanda wa Gaza. **PICHA: AFP**

# Wahouthi waapa kuishambulia Israel

**SANAA,** YEMEN

OFISA mmoja wa kundi la waasi wa Houthi nchini Yemen, anasema kundi hilo litaendelea kushambulia Israel katika kuwaunga mkono Wapalestina.

Siku chache zilizopita Israel ilifanya mashambulizi makali ya anga dhidi ya kambi za kijeshi nchini Yemen na kusababisha vituo vya umeme na miundo mbinu mbalimbali kuharibiwa.

Mohammed al-Bukhaiti aliiambia BBC kwamba Wahouthi watazidisha lengo lao la kijeshi dhidi ya Israeli hadi hapo itakomesha kile walichokitaja mauaji ya halaiki Ukanda wa Gaza.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema kipigo walichotoa jeshi lake kwa Yemen ni majibu kwa zaidi ya mwaka mmoja wa mashambulizi ya makombora na ndege zisizo na rubani yaliyofanywa na kundi linaloungwa mkono na Iran dhidi ya Israel.

Usiku wa kuamkia jana, waasi wa Houthi walirusha kombora jingine la masafa marefu kuelekea Israel, ambalo jeshi la Israel lilisema lilinaswa kabla ya kufika katika ardhi ya Israel.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alisema ana wasiwasi mkubwa kuongezeka kwa kasi kwa mashambulizi.

Pia ametaja mashambulizi katika uwanja wa ndege na bandari kuwa ya kutisha na kuonya kuwa yanaleta hatari kwa operesheni za kibinadamu katika nchi hiyo iliyokumbwa na vita.

Waasi wa Houthi, ambao wanadhibiti kaskazini-magharibi mwa Yemen, walianza kushambulia Israel na meli za kimataifa muda mfupi baada ya kuanza kwa vita kati ya Israel na Hamas Ukanda wa Gaza Oktoba 2023.

Israel imefanya mashambulio manne ya anga dhidi ya Wahouthi tangu mwezi Julai kulipiza kisasi kwa makombora 400 na ndege zisizo na rubani ambazo jeshi la Israel linasema yalirushwa kutoka Yemen, huku mengi yakidunguliwa

Marekani na Uingereza pia zimefanya mashambulizi ya anga nchini Yemen kujibu mashambulizi ya kundi hilo dhidi ya meli za kibiashara zinazopita kusini mwa Bahari ya shamu na Ghuba ya Aden.

**BBC**

# Bil. 3.16/- kutumika kuboresha afya, lishe

**Na Steven William** MUHEZA

DIVISHENI ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, kwa mwaka 2025/26 inatarajia kukusanya na kutumia Sh. bilioni 3.168 ili kugharamia utekelezaji wa mpango na bajeti.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk.Fani Mussa, alisema hayo juzi katika kikao cha maandalizi ya mpango kabambe wa afya kwa mwaka 2025/26 kilichofanyika katika ukumbi wa Hospitali ya Wilaya ya Samia.

Alisema mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Sh. 876,627,203 yakijumuisha mapato ya vituo vya huduma za afya yanayokadiriwa kufikia Sh. 462,700,000.

Dk. Mussa alisema katika mwaka 2023/24, divisheni ilikadiria kupata mapato na kutumia Sh. bilioni 3.598. Katika kipindi hicho, divisheni ilipokea Sh. bilioni 3.728 sawa na asilimia 103.6 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Alisema kiasi hicho kinajumuisha Sh. 389,749,812.78 mapato ya ndani sawa na asilimia 223.63 ya lengo la mwaka la Sh. 174,280,000.

Dk. Mussa alisema katika kipindi hicho, divisheni imetumia Sh. bilioni 3.426 kugharamia utekelezaji wa shughuli na miradi na Sh. milioni 4.59 zilivuka mwaka.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, alisema divisheni imepokea Sh. 767,441,921.08. Kati ya kiasi hicho, Sh. 192,528,604 ni mapato ya makusanyo ya vituo vya huduma za Afya ndani, sawa na asilimia 52.6 ya lengo la Sh. 366,050,000 na kwa kipindi cha robo ya kwanza, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya ni asilimia 90 kwa wastani kwa halmashauri

Alisema kwa kipindi cha Julai hadi Septemba, vituo vimepata bidhaa za afya kwa njia ya ruzuku kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD) zenye thamani ya Sh. 70,158,186.

**Dk. Mussa alisema katika mwaka 2023/24, divisheni ilikadiria kupata mapato na kutumia Sh. bilioni 3.598. Katika kipindi hicho, divisheni ilipokea Sh. bilioni 3.728 sawa na asilimia 103.6 ya bajeti iliyoidhinishwa.**

Pia alisema mwaka 2025/26, divisheni itaendelea kutekeleza vipaumbele 13 vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Mpango Kabambe wa Afya kwenye (CCHP Toleo la 5 la mwaka 2020.) na maelekezo mahususi ya Mwongozo wa Mipango na Bajeti wa Serikali wa mwaka 2025/26.

Mgeni rasmi katika mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Issa Msumari, alisema kumekuwa na tabia ya watumishi wa idara ya afya serikali inaleta fedha katika sekta hiyo, zinapelekwa katika vituo lakini hazitumiki mpaka mwaka unapita halafu zinarejeshwa tena serikali kuu mtindo aliosema hataki kuusikia kabisa.

Alisema lazima watumishi wa afya wajenge umoja wa kujaliana na kuthaminiana katika kazi na kwamba mtumishi anapotakiwa kupewa stahiki yake ya posho kutokana na mshahara wake apewe na si kuzungushwa.

# Waagizwa kuunda kamati ya maji

**Na Steven William,** MUHEZA

CHAMA Cha Mapinduzi CCM Kata ya Mtindiro wilayani Muheza, Tanga, kimewaagiza viongozi wa kijiji cha Kwabota Mnazi Mmoja kuunda kamati ya maji kwa ajili ya kusaidia kutoa huduma kwa wananchi na kulinda miundombinu katika mradi mpya wa maji.

Agizo hilo lilitolewa jana na Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Mtindiro, Timothy Kapesa, wakati akizungumza na wananchi.

Alisema katika kijiji hicho umetekelezwa mradi wa maji kwa ajili ya kuwaondolea adha wananchi kusaka maji visimani.

Kapesa alisema huduma hiyo ya maji imesogezwa kwa wananchi ikiwa ni Ilani ya Uchaguzi ya CCM kupitia serikali ya awamu ya sita kumtua mama ndoo kichwani.

Alisema mradi wa maji kijiji cha Kwabota Mnazi mmoja, umetumia fedha nyingi, hivyo kushauri viongozi waunde kamati ya maji kwa ajili ya kusaidia namna ya kutoa huduma na kulinda miundo mbinu ya maji.

Kapesa alisema mradi huo umetumia pesa nyingi kupitia serikali kuhakikisha huduma ya maji kwa kila mwananchi inamfikia kwa ukaribu.

Diwani wa Mtindiro, Mustapha Hatibu, alisema katika vijiji vyote vya kata hiyo tayari vimepata huduma ya maji, umeme, afya, barabara na huduma ya elimu.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Enzi vijana kuzamia meli, wengine waliishia Msasani



**Na Adam Fungamwango**

NCHI imetoka mbali sana hii. Unapoona maendeleo ya mtu mmoja mmoja, miundombinu ya sasa na vitu vingine unakuja kugundua kuwa Tanzania imepiga hatua sana.

Nakumbuka kipindi kile baada ya Vita vya Kagera, hali ya uchumi ilikuwa ngumu kiasi kwamba nchi ilipitia kipindi kigumu, hasa kuanzia mwaka 1980 na kuendelea hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990, yalipokuja mageuzi ya kiuchumi.

Ni kipindi ambacho hata vyakula ilikuwa shida. Unga, mchele, sukari, maharage, unga wa ngano vilikuwa vitu adimu kupatikana.

Nguo ndiyo kabisa ilikuwa utata mtupu. Kwa kweli hali haikuwa nzuri.

Kuna wakati Tanzania ilipata msaada wa unga wa mahindi kutoka Marekani wenye rangi ya njano. Wabongo kama kawaida yao wakauita unga wa 'Yanga.'

Ile rangi ya njano waliinasibisha na rangi inayotumiwa na timu ya mpira wa miguu nchini, Yanga.

Hiki ni kipindi ambacho kilisababisha waliokuwa vijana kwa wakati huo, kuanzia miaka 15 hadi 30, kutaka kuondoka nchini. Walitaka kuondoka kwa ajili ya kukimbia hali ya kiuchumi, hasa baada ya kumalizika vita hiyo ambayo Tanzania iliichapa Uganda.

Vilianza Oktoba 30, 1978 hadi Aprili 11, 1979. Vijana wengi hawakuwa na uwezo wa kuondoka nchini kutokana na kutokuwa na pasipoti wala nauli, wengi waliamua kuzamia meli kwa ajili ya kwenda nchi za Ulaya, mabara mengi na hapa Afrika, nchi waliyokuwa wakiihusudu ni Afrika Kusini, enzi za Makaburu.

Walitaka kuondoka ili kwenda ughaibuni ambako waliamini watapata kazi yoyote ile, pamoja na unafuu wa maisha kwenye nchi hizo.

Baadhi walifanikiwa na wengine hawakufanikiwa.

**Baadhi walifanikiwa na wengine hawakufanikiwa. Kazi yao kubwa ilikuwa kusubiri meli zinazoingia nchini na wao wanafanya ujanja na kuingia ndani ya meli hizo kujificha ili wasionekane na yeyote yule. Siku meli ikiondoka na wao wamo ndani.**

Kazi yao kubwa ilikuwa kusubiri meli zinazoingia nchini na wao wanafanya ujanja na kuingia ndani ya meli hizo kujificha ili wasionekane na yeyote yule. Siku meli ikiondoka na wao wamo ndani.

Mara nyingi mabaharia na manahodha wanakuja kujua kuna watu tayari wameshafika wakakokwenda au tayari wameshafika mbali.

Wale waliopata bahati ya kufika ughaibuni wengi wao walifanikiwa. Wengine hawakufanikiwa.

Waliorejea na mafanikio nyumbani, wakiwa na nguo za kisasa, viatu na hali nzuri kimaisha, mbwembwe zao, walichochea vijana wengi kuzidi kutaka kuzamia meli.

Bahati mbaya iliwapata baadhi yao walikuwa wakikamatwa na kutoswa baharini na kuliwa na samaki wakubwa.

Kuzamia meli sasa ikawa kama kamari.

Unaweza kufika unakokwenda au ukipata bahati unapata kazi melini na kuwa baharia au utoswe baharini.

Kuna stori nyingi kuhusu hilo, inasemekana kuna vijana walizamia meli na kukaa siku sita ndani akijua linakwenda, lakini kumbe bado lipo bandarini.

Walipoibuka walipojificha wakidhani limetua Sauzi, kumbe ipo Msasani, Mabaharia wakawakamata, wakawashusha kwenye boti na kuwarudisha bandarini.

Visa hivi na aina hii ya maisha ya wakati huo iliwafanya baadhi ya wanamuziki wa dansi kama kawaida yao kugusia eneo hilo.

Bendi ya Vijana Jazz, ilifyatua wimbo waliouita 'Ngapulila', ambao ulikuwa ukimzungumzia kijana mmoja aliyekuwa na ndoto ya kuzamia meli ili akapate maisha mazuri Ulaya kama baadhi ya wenzake.

Hata hivyo, rafiki yake alionekana kumuasa kwa kumwambia jambo hilo ni la hatari sana kwake, badala yake akae nchini na kujishughulisha na shughuli zingine za kujiingizia kipato. Wimbo ulitungwa na Adam Bakari.

"Rafiki yangu nakuaga mimi ee, nataka kuzamia meli niende ng' mbo kutafuta maisha ee, kwani naona maisha ya hapa nyumbani kaka ee yamenishinda.

Nakula kwa tabu, navaa kwa tabu, kulala kwangu gheto, basi naona shida tupu ee, shida tupu. Sina raha masikini eee, sina raha hata kidogo Ngapulila ee"

Rafiki yake naye akamjibu: "Maisha ya kuzamia melini yana hatari kubwa ee, kutoswa baharini na kupoteza maisha yako, Ngapulila ee, epukana na mawazo hayo ee, Ngapulila kaka, una hatari ee.

"Ngapulila mwenzio ameshikwa ughaibuni, kazamia meli na kukutwa na madawa ya kulevya na sasa yupo kifungoni, Ngapulila Ngapulila epukana na mawazo hayo ee, Ngapulila kaka, una hatari.

"Fanya kazi kwa bidii utapata kaka, tamaa ya kufika ng'ambo, imeponza wengi, wengine walijaribu, kuteka ndege nyara kutumia silaha za bandia, Ngapulila ee, una hatari ee."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-15

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AKAINGIZA mkono wake mfukoni na kutoa simu yake ya mkononi. Ni kama alikuwa anaangalia kama atapigiwa simu na watekaji. Mara tatu nzima zoezi lilikufa, au liliahirishwa baada ya kupigiwa simu akiambiwa arejee na mkoba wake kwani wamegundua kuwa wanafuatiliwa na polisi ili kukamatwa. Safari hii hakukuwa na kitu kama hicho. Ni kama Macky hakuamini.

Akavuta hatua taratibu kurudi nyuma.

Alipofika barabarani akavuka na kuondoka eneo la tukio haraka kama alivyoamriwa na watekaji. Kitu kilichobaki kichwani kwake ni kesho kupata mtoto wake Macaire.

Watekaji walimwambia kama zoezi likifanikiwa atapigiwa simu saa nne kamili asubuhi na kuelekezwa ni wapi aende akamchukue mtoto wake, akiwa salama salimini.

Kitu ambacho Macky alikuwa na uhakika nao ni kwamba watekaji watakuja kuuchukua mzigo wao baadaye.

Hakujua kuwa kuna watu watano kwenye eneo hilo walikuwa wakimwangalia kwa makini na wakifuatilia kila alichokuwa akikifanya.

Aliyekuwa makini zaidi kuliko wote ni Eddy. Alikuwa tayari ameshatoa bastola yake ambayo ina kiwambo cha kuzuia sauti.

Alikuwa tayari kwa lolote litakalotokea, au yoyote aliyetaka kumdhuru Macky.

Baada ya kuondoka, kilichobaki ni watekaji kusogelea mkoba na kuchukua pesa zao shilingi milioni 15 ambazo walizihitaji ili wamuachie mtoto Macaire.

Alisikia kitu kama mguno au mbinja. Ikambidi awe makini zaidi. Hakupepesa macho kabisa. Macho yake yalitazama kodo kama samaki aliyekaangwa au aliyewekwa kwenye jokofu.

Ghafla aliona yule aliyekuwa kwenye kibanda ambacho mchana mama mtilie huuzia wafanyakazi wa eneo lile chakula alitoka.

Akavuka barabara kwa uangalifu. Tayari Eddy alijua kuwa huyu ndiye aliyepewa kazi ya kwenda kuuchukua mkoba wenye pesa, huku wenzake wote wakiwa wanamlinda. Akatembea taratibu na kwenda moja kwa moja kwenda mkoba. Akainama na kuuinua mkoba ule.

Kitu ambacho hakufanya ni kufungua zipu ili kuangalia. Nadhani muda haukuruhusu, pia hawakujisahaulisha kuwa lilikuwa ni eneo la hatari.




Bado hawakuwa na uhakika wa usalama wao juu ya polisi ambao mara mbili.

Aliweka begani na kuondoka nao, akivuka barabara na kurejea tena ndani ya kibanda.

Awali akili ilimtuma Eddy ampige risasi ya mguu.

Hata hivyo wazo likamjia kuwa akifanya hivyo atakuwa ameshawatangazia wenzake kuwa kuna mtu au watu wengine zaidi yao eneo hilo na lengo lao si jema kwao, hivyo ingeweza kumpa ugumu wa kufanya kazi hiyo kwa ufasaha.

Alitulia kwanza. Sekunde chache baadaye aliona yule mmoja aliyekwenda kujificha upande wa kushoto akitoka na kuelekea kule ambako mwenzake walikwenda.

Mpaka wakati huo usiku ulikuwa unaelekea kuwa mkubwa na utulivu wa hali ya juu uliokuwa unasababisha sehemu hiyo indelee kutisha kama kuzimu.

Alichoona kitu cha kuhimu zaidi ni kudili na mtu ambaye alikuwa karibu yake pale.

Hatua 12 tu mbele yake kulikuwa na yule aliyejibanza hapo. Alijua akianza na huyu ataifanya kazi hiyo kwa urahisi sana.

Alianza kutambaa kikomandoo. Alionekana kama mamba anayemnyatia kitoweo.

Kwa namna ambayo ilimfanya jamaa aliyejificha pale kutohisi chochote hadi alipofika hatua kama tano au nne hivi.

Alisikia kama kuna kitu kinachecheza nyuma yake. Akageuka ghafla.

**Ni wakati wale wa upande wa kulia nao walitoka na kuelekea walipo wenzao. Hawa sasa hawakuonekana na wasiwasi kabisa kwani walishaanza kuhisi kuna amani.**

Alikuwa amechelewa. Eddy alinyanyuka ghafla na kumrukia kabla hajafanya chochote, akamuangusha chini kama wanavyofanya wachezaji mieleka.

Hakutaka kupigana juu ili wenzake wasione au kuhisi kama kuna chochote kibaya. Alimbana kwa kabali ya nguvu kwa sekunde kadha hadi alipoona kaishiwa nguvu.

Haraka alitoa kichupa chake kidogo cha poda ya sumu.

Kama nilivyosema awali kuwa sumu hiyo haimuui binadamu ila humfanya apoteze fahamu kwa siku tatu au nne. Mwenyewe alikuwa amevaa glovu nyembamba mikononi.

Aliminina kidogo na kumuwekea mdomoni na puani kidogo ili aivute.

Hakutaka hata kumtazama tena kwani alijua kazi yake hapo imekwisha.

Ni wakati wale wa upande wa kulia nao walitoka na kuelekea walipo wenzao.

Hawa sasa hawakuonekana na wasiwasi kabisa kwani walishaanza kuhisi kuna amani.

Haraka Eddy alirudi alikotoka akiwa anatambaa mpaka eneo ambalo aliona hata akinyanyuka hawatomuona.

Alirudia njia ile ile ambayo alijia. Kilichompa ugumu sasa ni kuvuka barabara.

Alijua akifanya hivyo wakamuona. Akabaki amekificha kwenye kichaka. Mara wote watatu walitoka kwenye kibanda.

Walionekana kama wanaulizana kuhusu mwenzao kutoonekana. Kwa bahati nzuri wakavuka barabara kuu ya kutoka Kigamboni kwenda Tuangoma kwenda kumtafuta mwenzao. Walionekana kutokuwa na wasiwasi kwani mpaka muda ule hakukuwa na dalili ya polisi wala kitu chochote cha kuwatia hofu. Hata kutoonekana kwa mwenzao waliona huenda amepata tatizo la kawaida.

"Katumbukia shimoni nini maana huku kuna mashimo kweli." Alisikika mmoja. "Angepiga kelele." Mwingine aliitikia.

Wakati wanabishana. Kwa kasi ya umeme, Eddy alivuka upande ule ambao walikuwa awali. Alizunguka mpaka kwenye kile kibanda. Alisubiri kwa dakika mbili, akawaona wanarejea.

"Yule ameshaumwa na nyoka, ameshakufa. Kwa sababu mzigo tumeshapata na kuna tatizo lolote hatuwezi tena kumbeba au kufanya chochote tuondokeni, kwani hili jambo tulilokuja kulifanya ni la hatari kama tukileta mbwembwe hapa tutakuja kukakamatwa," aliongeza mmoja wao kwa sauti nzito akionekana kama ndiye kiongozi wa kundi.

"Dah, Pius hatunaye tena." Mmoja alidakia. "Hii inaitwa ajali kazini. Tuondokeni upesi." Akaamuru kiongozi wao.

Kitu ambacho Eddy alifahamu ni kwamba hawakuja kwa daladala wala kwa miguu. Kuna sehemu ambayo watakuwa wameweka gari yao.

Akaamua kuwafuata nyuma nyuma kwa uangalifu. Wala hawakwenda mbali sana.

Ni kama mita 500 tu. Ni kule ambako barabara ya vumbi imekata. Eddy alikuwa amejiandaa na awamu wa pili ya mapambano. Hii ndiyo itakuwa kubwa zaidi kuliko ile ya kumzimisha Pius kwa sumu. Kitu ambacho alichokihitaji pale ni kuhakikisha hakuna yeyote atakayeondoka pale.

Alitaka pia kuuchukua ule mkoba wa pesa wenye Shilingi milioni tano, badala ya milioni 15 urejee mikononi mwake.

Kwa hali ya kawaida haikuwa kazi rahisi hata kidogo. Walitumwa au kujituma kuchukua hizo pesa nao walikuwa wamejidhatiti. Hawakuwa dhaifu hata kidogo kwani ni wataalamu wa hizo kazi.

Kwake Eddy alishapanga nini afanye ili alianzishe na kazi ya kupambana nao pamoja na kuurudisha mkoba mikononi mwake.

**Itaendelea Jumapili**

# BEYONCE APATA PRESHA JAY-Z KUTOONEKANA

MWANAMUZIKI wa Marekani, Beyonce, ametumbuiza katika mchezo wa mpira wa kikapu FNL, huku akikabiliwa na shinikizo la kumtaka aeleze aliko mume wake, Jay-Z.

Jay-Z ambaye ana dili kubwa la kusimamia burudani katika mchezo huo, hakuonekana wakati Beyonce akitumbuiza.

Hata hivyo, Beyonce alifanikiwa kuwapagawisha mashabiki wa mchezo huo kwa kuimba vibao kutoka kwenye albamu yake ya hivi karibuni, Cowboy Carter.

Siri ya kutokuwepo kwa Jay-Z inaweza kuhusishwa na masuala ya kisheria yanayoendelea kuhusu kuhusika na vitendo vya unyanyasaji wa kingono.






# MADEE ABEBA UZALENDO UINGEREZA

MWANAMUZIKI mkongwe wa Bongo Fleva, Madee, yupo nchini Uingereza na katika kitendo cha kipekee msanii huyo akiwa katika uwanja wa timu ya soka ya Arsenal, amepeperusha bango lenye picha ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Madee ameonekana akiwa na watu wengine ndani ya kiwanja hicho wakiwa wamebeba bango hilo likiwa na picha ya Rais Samia na Bendera ya Tanzania.

Aidha, msanii huyo amekua akisafiri mara kadhaa kwenda Uingereza kwa ajili ya kutazama timu yake ikicheza michezo ya ligi kuu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**JUVE HAIMTAKI RASHFORD**
KLABU ya Juventus imekataa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na England, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, lakini badala yake wanamtaka mshambuliaji mwenzake kwenye kikosi hicho, Joshua Zirkzee mwenye miaka 23, ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi. (**Sun**)

**ZUBIMENDI KUMRITHI RODRI**
MANCHESTER City inapanga kumsajili Martin Zubimendi wa Real Sociedad na Hispania mwenye umri wa miaka 25 ili kuziba pengo la jeraha la Rodri mwenye umri wa miaka 28.(**Football Insider**)

**MUSIALA AWINDWA ULAYA**
MANCHESTER City, Liverpool, Real Madrid na PSG zote zinafikiria iwapo zitamnunua kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 21, ambaye thamani yake ni karibu pauni milioni 150 Januari. (**Caught Offside**)

**MUANI ATAKIWA MAN UNITED**
KOCHA Ruben Amorim ana matumaini Manchester United inaweza kumsajili fowadi wa PSG na Ufaransa, Randal Kolo Muani mwenye umri wa miaka 26 Januari licha ya ushindani kutoka kwa Chelsea, Tottenham na Arsenal. (**TeamTalks**)

**ARSENAL, UNITED ZAMTAKA CUNHA**
KLABU ya Wolves haitakaribisha ofa kwa fowadi wao wa Brazil, Matheus Cunha mwenye umri wa miaka 25 Januari, huku Arsenal na Manchester United zikimwania. (**Mirror**)

**JUVENTUS KUMSAJILI TOMORI**
JUVENTUS inataka kumsaini beki wa kati wa England, Fikayo Tomori mwenye umri wa miaka 27 kutoka AC Milan. (**La Gazzetta dello Sport**)

**MCATEE ANYATIWA MAN CITY**
KLABU ya Manchester City inataka kumnunua James McAtee mwenye umri wa miaka 22 huku Nottingham Forest, West Ham, Brentford, Bayer Leverkusen na Fiorentina zote zikiwa na nia ya kumsajili kiungo huyo wa kati wa England chini ya miaka 21. (**Telegraph**)

**LEWIN KWENYE RADA EVERTON**
MSHAMBULIAJI wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27 anaweza kukubaliana mkataba wa awali na Fiorentina Januari huku Newcastle United na West Ham pia zikimtaka. (**TeamTalks**)

**LIVER KUMPIGA BEI KELLEHER**
LIVERPOOL ipo tayari kumuuza mlinda lango wa Jamhuri ya Ireland, Caoimhin Kelleher mwenye umri wa miaka 26, kwa bei ifaayo msimu ujao huku Newcastle United ikifuatilia hali yake. (**TeamTalks**)

**ZAGA ASAKWA LIGI YA MAREKANI**
WINGA wa Galatasaray na Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 32 ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Lyon, anaweza kutua kwenye Ligi Kuu ya Marekani. (**Mail**)

**MAN UNITED KUTUA ANTWERP**
KLABU ya Manchester United inataka kufanya mazungumzo na Royal Antwerp kwa ajili ya kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Ubelgiji, Senne Lammens mwenye umri wa miaka 22. (**Telegraph**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ANTONY MAMBO MAGUMU UNITED

**MANCHESTER,** England

WAKALA wa winga wa Manchester United, Antony amefichua kuwa klabu hiyo haijatoa dalili zozote za kutaka kuachana na mchezaji huyo katika dirisha la usajili la Januari.

Antony aliyesajiliwa kwa pauni milioni 82 kutoka Ajax mwaka 2022, ameshindwa kutimiza matarajio na kupoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza chini ya kocha wa zamani Erik ten Hag, huku kocha wa sasa Ruben Amorim akikataa kumrejesha mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kwenye kikosi chake cha kwanza.

Kwa hiyo, ripoti zimedai kwamba United tayari imeamua kukata uhusiano na Antony wakati wa dirisha la usajili la msimu wa baridi litakapofunguliwa.

Lakini wakala wa Antony, Junior Pedroso, alithibitisha kuwa United haijaonesha nia yoyote ya kutaka kumuachia aondoke.

**● ● ● Wakala wa nyota huyo amefichua kuwa mpaka sasa klabu hiyo....**

**"Ndiyo, klabu nyingi zimetutafuta kwa ajili ya usajili wa Antony Januari," alisema akimuambia Fabrizio Romano.**

"Klabu zilitaka kuelewa hali ya Antony, kwa hiyo naweza kuthibitisha kwamba kuna nia thabiti.

"Kusema ukweli, Manchester United haijawahi kuonesha nia yoyote ya kumuuza au kumtoa Antony kwa mkopo.

"Hatujawahi kupokea mawasiliano ya aina hii hadi sasa. Uongozi wa Man Utd haujawahi kutuambia kwamba wanataka Antony aondoke."

Hata hivyo, Pedroso alikiri kuwa watakuwa tayari kusikiliza United ikiwa Mashetani Wekundu watapendekeza kuhama kwa mkopo Januari.

"Naweza kusema kwamba mustakabali wa Antony unahusishwa sana na maslahi ya Manchester United," alisema.

"Ikiwa klabu inaona lingekuwa jambo zuri kumtoa kwa mkopo Antony Januari ili apate dakika zaidi na kurejesha makali yake na imani kwa timu, tutafanya kazi pamoja katika chaguo hilo.

"Vinginevyo, Antony anafanya bidii kurejesha nafasi yake na kuonesha ujuzi wake bora chini ya kocha mpya Ruben Amorim."

## HABARI MICHEZO



# SAKA KURUDI UWANJANI MACHI

**LONDON,** England

BUKAYO Saka amefanyiwa upasuaji wa jeraha la misuli ya paja na anatarajiwa kuwa nje ya uwanja hadi Machi mwakani, kocha wa Arsenal, Mikel Arteta amethibitisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 aliumia msuli wa mguu wake wa kulia wakati wa kipindi cha kwanza cha ushindi wa 5-1 Jumamosi iliyopita dhidi ya Crystal Palace.

"Amefanyiwa upasuaji, kila kitu kilikwenda sawa," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari baada ya ushindi wa Arsenal dhidi ya Ipswich juzi.

"Lakini kwa bahati mbaya atakuwa nje kwa wiki nyingi sana."

Arteta aliongeza, "Nilisema 'wiki nyingi' kwa hiyo nadhani itakuwa zaidi ya miezi miwili.

"Sijui ni muda gani haswa. Nadhani itategemea jinsi atakavyokuwa akipona, huanza kupona wiki ya kwanza au zaidi na hiyo ni ngumu sana kusema.

Washikabunduki hao walimtumia Kai Havertz kama mbadala wa Saka na alifunga bao na kuwafanya Arsenal kujiweka nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi, pointi sita nyuma ya vinara wa Ligi Kuu, Liverpool.

Arteta alikuwa na furaha zaidi kuhusu hali ya Raheem Sterling baada ya awali Arsenal kuhofia winga huyo pia angekaa nje kwa kipindi kirefu kutokana na tatizo la goti.

"Habari ya Sterling nadhani ni bora," alisema. "Lazima tuone wiki hii jinsi anavyobadilika, lakini tulitarajia jeraha la goti lingechukua muda mrefu zaidi kuliko jinsi goti lilivyobadilika siku chache zilizopita."

# De Jong hana mpango na Saudia

**BARCELONA,** Hispania

WAKALA wa Frenkie de Jong amekanusha habari zinazomhusisha kiungo huyo na kuhamia Saudi Arabia na amesema bado anataka kuendelea kucheza Barcelona.

Ripoti nchini Hispania zilidai kuwa Ali Dursun, ambaye anamwakilisha De Jong, alifanya mazungumzo na pande kadhaa za Saudia kuhusu uwezekano wa uhamisho wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi.

"Habari kuhusu uwezekano wa kuhamia Saudi Arabia ni upuuzi mtupu," alisema Dursun akiiambia De Telegraaf.


"Wanavuruga tu matarajio ya kweli ya Frenkie: kung'ara Barca, klabu anayoipenda na mahali anapojisikia yuko nyumbani.

"Pande zote mbili zinafurahi na, ni nani anayejua, labda tunaweza kukaa pamoja kwa muda mrefu zaidi."

De Jong mwenye umri wa miaka 27, alijiunga na Barca kutoka Ajax mwaka 2019 na ana mkataba na klabu hiyo ya Katalunya hadi 2026, lakini kwa sasa anapitia kipindi kigumu zaidi tangu ahamie Hispania.

Alikosa miezi michache ya kwanza ya msimu kutokana na jeraha la kifundo cha mguu alilolipata Aprili mwaka jana na hatimaye akarejea kwenye kikosi cha kwanza Oktoba.

# Ronaldo: Ningekuwa mmiliki Man United, ningerekebisha mambo



**DUBAI,** Falme za Kiarabu

CRISTIANO Ronaldo amesema kwamba, matatizo ya Manchester United hayamhusu kocha mpya Ruben Amorim na anaamini angeweza kuyarekebisha iwapo angekuwa mmiliki wa klabu hiyo.

Amorim amepoteza mechi tano kati ya 10 akiwa kocha wa United ikiwa ni pamoja na mechi nne kati ya tano zilizopita kwenye Ligi Kuu England na alisema kabla ya mchezo ujao dhidi ya Newcastle United kwamba kibarua chake si salama.

Lakini Ronaldo, ambaye alifunga mabao 145 katika vipindi viwili vya United amewakosoa wamiliki wa klabu hiyo, pamoja na mambo mengine katika miaka ya hivi karibuni na akabainisha raia mwenzake huyo wa Ureno hapaswi kulaumiwa.

"Ligi Kuu England ni ligi ngumu zaidi duniani," alisema Ronaldo, ambaye kwa sasa anachezea Al Nassr ya Saudi Arabia wakati wa halfa ya tuzo za Globe Soccer huko Dubai, Ijumaa.

"Timu zote ziko vizuri, timu zote zinapambana, timu zote zinakimbia, wachezaji wote wana nguvu, mpira wa miguu sasa hivi ni tofauti, hakuna michezo rahisi tena.

"Nilisema hivi mwaka mmoja na nusu uliopita, na nitaendelea kusema: Tatizo sio makocha.

"Tatizo la Manchester United ni lile lile. Tatizo sio mara zote kocha. Ni zaidi ya hapo.

"Ningekuwa mmiliki wa klabu, ningeweka mambo wazi na kurekebisha kile ninachofikiri ni kibaya."

"Mimi si kocha. Sitaweza kamwe kuwa kocha, rais wa klabu? Hapana. Labda mmiliki wa klabu," alisema.

"Itategemea wakati, fursa sahihi."

Alipoulizwa kama alikuwa na lolote akilini, Ronaldo alijibu kwa fumbo: "Bado.."

Lakini akihojiwa kuhusu kuwasiliana na familia ya Glazers moja kwa moja, Ronaldo alisema, "Bado mimi ni mdogo sana, nina mipango na ndoto nyingi mbeleni.

"Lakini zingatia maneno yangu, nitakuwa mmiliki wa klabu kubwa. Hakika."

Ronaldo aliondoka United mwaka wa 2022 kufuatia kutofautiana hadharani na Erik ten Hag na mahojiano ya televisheni ambapo Ronaldo alitoa madai mengi, ikiwa ni pamoja na kwamba wamiliki familia ya Glazer hawajali klabu.

Tangu kuondoka kwa Ronaldo, Ineos Group ya Sir Jim Ratcliffe imechukua udhibiti wa uendeshaji wa soka, wakati Ten Hag alitimuliwa kabla ya kuajiriwa kwa Amorim.

Lakini Ronaldo bado anahisi matatizo yanaendelea.

Alipoulizwa kuhusu Amorim, fowadi huyo wa Ureno alisema: "Alifanya kazi nzuri sana nchini Ureno na klabu yangu ya Sporting. Lakini Ligi Kuu England ni tofauti, ni ligi tofauti, ni ligi yenye ushindani mkubwa zaidi duniani."

# TAOUSSI AFICHUA KILICHOIPONZA JKT TANZANIA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Rachid Taoussi, amesema haikuwa rahisi kuifunga JKT Tanzania lakini wamefanikiwa kufanya hivyo kutokana na kuifahamu vyema timu hiyo inavyocheza baada ya kukutana nayo katika mchezo mmoja wa kirafiki walioocheza kwenye kalenda ya FIFA.

Akizungumza mara baada ya kumalizika kwa mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo dhidi ya JKT Tanzania, kocha huyo alisema ushindi wa mabao 3-1 walioupata umechangiwa zaidi na kuifahamu sana timu hiyo aina yake ya uchezaji kwani walishawahi kucheza nao mechi moja ya kirafiki, hivyo hakuwa na kazi sana ya kupanga mpango mkakati wa kuisulubu.

"JKT Tanzania ni timu nzuri, ina wachezaji wenye vipaji na wenye nguvu, si jambo rahisi sana kuwafunga idadi hii ya mabao, niliingia na mfumo mwingine kipindi cha kwanza, nilipobadilisha wachezaji kipindi cha pili nilibadilisha tena mfumo, tukawa makini kuhakikisha hawatushambulii kwa kushtukiza kwa sababu wana wachezaji wenye kasi wanapotoka kwenye eneo lao kwenda kushambulia, kusema kweli ninajivunia wachezaji wangu kwani hii ni mechi ya 10 mfululizo tunapata ushindi, hatumbweteki tutaendelea hivi hivi," alisema.

Mabao ya Azam juzi yaliwekwa wavuni na Paschal Msindo dakika ya 36 na Idd Suleiman 'Nado', dakika ya 63 na 71 huku lile la JKT Tanzania ikifungwa na Said Ndemla dakika ya 13 ambalo lilikuwa la kwanza kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Ushindi huo umeiwezesha Azam kufikisha pointi 36 sawa na Yanga, lakini ikiendelea kubaki nafasi ya tatu kutokana na uwiano wa mabao ya kufunga na kufungwa.

Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza timu hizo zilipocheza kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Agosti 28 mwaka huu, timu hizo zilitoka suluhu.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, alisema kipindi cha pili hawakuwa bora, hasa kwenye ukabaji.

"Kipindi cha pili hatukuwa makini kwenye kukaba, hatukuwa bora wakati tukiwa na mpira na hata tulipopoteza mpira, kama una mpira halafu ukapoteza kizembe, mpinzani anaweza kukuadhibu.

Matokeo yake tumefungwa mabao mawili ya haraka ambayo yaliua mechi, tumefungwa michezo miwili mfululizo, hivyo inabidi twende tukajipange upya," alisema kocha huyo.




Meneja wa Bidhaa wa Yas, Eginga Mohamed (kulia) akimkabidhi mfano wa hundi Chiku Rashidi (kushoto) baada ya kuibuka mshindi wa kampeni ya 'magifti'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkazi Dar aibuka mshindi Magifti

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Dar es salaam, Chiku Rashid juzi ameibuka mmoja wa washindi wa kampeni ya Magift inayoendeshwa na kampuni ya Yas.

Chiku ni miongoni mwa waishindi wa shilingi milioni moja katika droo ya saba iliyochezshwa juzi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi ya kiasi hicho, Chiku ambaye ni mfanyabiashara wa nguo, amesema zawadi hiyo kwake imekuja wakati muafaka kutokana na majukumu aliyonayo.

Alisema sehemu ya pesa hiyo ataongeza kwenye mtaji wake wa nguo .

"Nawashauri watumiaji wenzangu wa simu kutodharau michezo kama hii, pesa hizi zitanisaidia sana kwenye shughuli zangu," alisema Chiku.

Kwa upande wake, Meneja wa bidhaa wa kampuni hiyo, Eginga Mohammed amewataka wananchi kushiriki kuwania zawadi wanazozitoa katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka.

"Hii ni wiki ya saba kuchezeshwa droo na bado wiki sita, wananchi wachangamkie fursa hii ya kushinda zawadi mbalimbali," alisema Mohamed.

# JKT: Tunafanyia kazi mapendekezo ya Kocha

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa klabu ya JKT Tanzania, umesema tayari wameanza kufanyia kazi mapendekezo ya benchi la ufundi la timu hiyo katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire alisema baada ya uongozi kumaliza kuyapitia mapendekezo hayo sasa wameanza kuyafanyia kazi kwa lengo la kuimarisha timu na kuwa na kikosi bora.

"TUmepokea mapendekezo ya Mwalimu na tayari yameanza kufanyiwa kazi, kila kitu kikikamilika tutatoa taarifa rasmi, alisema Bwire.

Alisema huwa hawakurupuki kufanya usajili bali wanasajili wachezaji ambao wataongeza ushindani ndani ya timu yao.

Bwire, alisema wanasubiri wakamilishe kila usajili ndipo waanze kuwatangazia watanzania pamoja na wadau wa soka wawafahamu nyota waliowasajili.

"Tunaomba mashabiki wetu wawe watulivu, tutakapomaliza usajili wetu tutatoa taarifa, malengo tuliyonayo ni makubwa, alisema Bwire.

# Shimbata 'wamuangukia' Rais Samia

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la mchezo wa Bao Tanzania (Shimbata) limemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwasaidia shilingi milioni 20 kwa ajili ya kusaidia gharama za matibabu ya kiongozi wa Shirikisho hilo, Mande Likwepa ambaye amelazwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi habari juzi, Mjumbe wa Shirikisho hilo, Rashid Kayumbo, alisema Likwepa ambaye ni rais wa Shirikisho hilo amelazwa kwenye hospitali hiyo tangu Jumanne iliyopita akisumbuliwa na matatizo ya moyo.

Alisema alianza kuugua tangu mwezi Oktoba mwaka huu siku chache baada ya kurejea nchini akitokea Kazakhstan alipokwenda kwa ajili ya shughuli za mchezo huo.

"Sisi kama Shimbata tunamuomba Rais Samia Suluhu Hassan aguswe na kukubali kumsaidia gharama za matibabu kiongozi wetu kwani Shirikisho letu halina uwezo wa kulipa gharama hizo, alisema Kayumbo.

Alisema Rais alikubali kuwasapoti wakati wote ndani na nje ya nchi kuhakikisha mchezo wa bao unafika kwenye maono ya ndoto na kiu ya Mwalimu Julius Nyerere ambapo mwaka huu walifanikiwa kwenda Kazakhstan kushiriki mashindano ya mchezo huo.

Alifafanua kuwa mafanikio waliyoyapata katika jitihada za kukuza na kueneza mchezo huo ndani na nje ya nchi, ni kutungwa kwa sheria zake kwa Lugha ya kingereza na Kifaransa.

Aliwaomba watanzania pamoja na wadau mbali mbali wa michezo hapa nchini kumuunga mkono kiongozi wao huyo ili aweze kurudi kuendelea na majukumu yake.

# Yanga kuwapa mashabiki...

INATOKA UK. 24

Kocha wa timu hiyo, Mohamed Muya, amekiri kuwa wanakwenda kucheza mechi ngumu dhidi ya timu bora ya Yanga, lakini haiwaondolei ari ya kupambana ili kupata ushindi.


"Tunaiheshimu Yanga, ni moja kati ya timu nzuri na kubwa kwenye nchi hii ambazo zimekuwa na mwendelezo mzuri, imesajili vizuri, lakini ni wakati wetu sasa timu za madaraja ya kati kuonyesha tumekua kiasi gani, tunapokwenda kumkabili adui tunaangalia nguvu yake na mapungufu yake, tumeiangalia, tumewapa mbinu wachezaji wetu wa kuikabili," alisema kocha huyo.

Fountain Gate kwa sasa ipo nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikikusanya pointi 20.

Michezo

Jumapili Desemba 29, 2024

Nipashe



## Antony mambo magumu Man United

UK. 21



Kiungo wa Simba, Fabrice Ngoma (kulia) akiruka juu kufunga bao pekee kwa timu yake kwenye mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Singida Black Stars jana kwenye uwanja wa CCM Liti mkoani Singida. Simba ilishinda 1-0. **PICHA: SIMBA**

# Yanga kuwapa mashabiki zawadi ya kufunga mwaka

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu, Yanga leo watashuka kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam kucheza mechi ya mwisho ya Ligi Kuu kwa mwaka huu huku wakiahidi kuwapa wanachama na mashabiki wa timu hiyo zawadi ya ushindi kwa ajili ya kuuaga mwaka 2024.

Nahodha ya timu huyo, Bakari Mwanyeto amewataka wanachama na mashabiki wa Yanga kumiminika uwanjani kwa wingi ili kuwapa sapoti ya kuwashangilia na wao watawapa zawadi ya ushindi ili washerehekee vyema kuuaga mwaka huu.

Yanga itacheza dhidi ya Fountain Gate katika mchezo ambao kama itashinda itafikisha pointi 39, ikimaliza mechi zake za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sead Ramovic amesema kwa mara nyingine tena wanakwenda kucheza mchezo mgumu, lakini kupambana na kujituma kwao ndiko kunaweza kuwapa ushindi kwenye mchezo huo.

"Tunakwenda kucheza mechi nyingine ngumu, tunataka kuonyesha watu nini tunafanya, nimesoma timu pinzani ni nzuri, ila kwa sasa tunajiangalia sisi nini tutakwenda kuoonyesha uwanjani kwa ajili ya kushinda na kupata pointi tatu.

Tunajua wanakuja na mfumo wa kukaa nyuma na kutushambulia kwa kushtukiza kitu ambacho ni hatari, lakini kujituma na nidhamu ndiyo kitu pekee ambacho kinaweza kutupa ushindi leo, tunataka kuitawala mechi," alisema kocha huyo.

Mwamnyeto, alisema kazi kubwa watakayoifanya leo upande wa mabeki ni kuhakikisha washambuliaji wao hatari hawagusi nyavu zao.

"Tunajua Fountain Gate ni moja kati ya timu zenye safu kali ya ushambuliaji, kwa hiyo mimi na mabeki wengu tunakwenda kufanya kazi ya kuwazuia ili wasilete madhara, ikiwezekana wasiguse nyavu zetu.

Fountain Gate ina mastraika, Selemani Mwalimu mwenye mabao sita, na Edgar William ambaye ana mabao matano.

Timu hiyo kwa sasa inashika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu kwa kufunga mabao mengi zaidi. Simba ikiongoza kwa mabao 30, Yanga mabao 27, Azam ikiwa imefikisha 25, Fountaig Gate ikiwa na mabao 24.

INAENDELEA UK 23

# Simba kumaliza mwaka kileleni

## Yaiduwaza Singida Black Stars nyumbani, Ngoma apeleka furaha kwa....

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa dakika tatu kabla ya mapumziko na kiungo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Fabrice Ngoma jana liliiwezesha Simba kupata ushindi muhimu wa bao 1-0 dhidi ya Singida Black Stars katika mchezo mkali uliotawaliwa na rafu na mabavu kwenye uwanja wa Liti mkoani Singida.

Kona iliyopigwa na Jean Ahoua iliunganishwa kwa kichwa na Ngoma na kujaa nyavuni huku ukiwaacha wachezaji wa Singida Black Stars wakiongozwa na golikipa wake, Metacha Mnata kumzonga mwamuzi wa mchezo huo, Shomari Lawi wakilalamika golikipa huyo kuchezewa faulo kabla ya mfungaji kufunga.

Metacha alitokea na mpira huo wa kona kwa lengo la kwenda kuucheza lakini aliukosa na Ngoma kuukwamisha nyavuni.

Ushindi huo unaifanya Simba kujihakikishia kuongoza msimamo wa Ligi Kuu ikifikisha pointi 40 na itakaa kilele hadi mwakani, kwani hata kama Yanga ikishinda mchezo wa leo dhidi ya Fountain Gate unaotarajiwa kuchezwa Uwanja wa KMC Complex itafikisha pointi 39.

Ratiba ya Bodi ya Ligi inaonesha baada ya mechi za leo, michezo inayofuata itapigwa kuanzia Januari 20 mwakani.

Simba imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza ikikusanya jumla ya pointi hizo na kuwa kilele mwa msimamo wa Ligi Kuu, ikishinda michezo 12, sare moja na kupoteza mchezo mmoja huku ikifunga mabao 31 na wenyewe kuruhusu mabao matano.

Aidha, Simba imefanikiwa kushinda michezo yake yote ya ugenini katika mzunguko wa kwanza ambapo imecheza michezo saba na kushinda yote.

Mechi ya jana ilianza kwa matumizi makubwa ya nguvu, hasa Singida Black Stars ambao walionekana kutaka kupunguza kasi ya Simba huku mara kwa mara wakiwa wanamzonga mwamuzi, Lawi.

Simba ingeweza kujipatia bao mapema tu dakika ya saba, pale Yusuph Kagoma alipopata nafasi ya kuingia ndani ya eneo la hatari na kuachia shuti kali ambalo hata hivyo lilipanguliwa na kipa Metacha na kuzagaa langoni, huku Steven Mukwala akipishana nao.

Dakika mbili baadaye, Kibu Denis naye alipata nafasi akiwa nje kidogo ya boksi, shuti lake la mguu wa kushoto lilibabatiza mabeki wa Singida na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Kosakosa kwenye lango la Singida zilienddelea dakika 31, Kibu akimuwekea pasi ya kifua Mukwala ambaye aligeuka ghafla na kupiga shuti lililompita kipa Metacha, lakini ukatoka nje sentimeta chache.

Singida ilifanya shambulio la hatari langoni mwa Simba dakika ya 36, pale mshambuliaji wake, Elvis Rupia alipomzidi mbio mbio beki Che Fondoh Malone lakini shuti lake lilipaa juu ya lango.

Baada ya kufungwa bao wachezaji wa Singida walionekana kutoka mchezoni na kama wachezaji wa Simba wangekuwa watulivu wangeweza kupata mabao mawili ya haraka, dakika ya 43 na 44 ikiwemo 'tik-tak' ya Kibu ambayo ilitoka juu kidogo ya lango.

Sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko, kipa wa Simba Moussa Camara alifanya kazi ya ziada alipodaka mpira wa kichwa kutoka kwa Rupia, akiunganisha krosi kutoka kwa Marouf Tchakei.

Kipindi cha pili wenyeji walikuja kwa kasi kwani dakika tatu baada ya kuanza kipindi cha pili, Rupia anayeongoza kwa upachikaji mabao kwenye Ligi Kuu akiwa na mabao manane, alipata nafasi ya kupiga shuti akiwa karibu na lango, lakini Camara kwa mara nyingine alifanya kazi ya ziada kuudaka mpira huo.

Timu zote zilifanya mabadiliko kipindi cha pili lakini haikuongeza wala kupunguza chochote kwenye mchezo huo.

Matokeo hayo yanaibakisha Singida Black Stars kwenye nafasi ya nne ikibakia na pointi 33 baada ya kucheza michezo 16.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >